SUPA JACKPOT
TZS. 1,077,433,324
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Kortini** madai ya kukutwa na meno ya tembo

UKURASA 3



UBUNIFU wa vitu kuanzia bidhaa na huduma mbalimbali ni miongoni mwa vipaji ambavyo kila binadamu huzaliwa navyo.

Ingawa kazi za ubunifu na ugunduzi zinafanyika, changamoto ni namna ya kuziendeleza, kuzibadili kuwa fursa na kuleta suluhisho kwenye matatizo ya jamii na taifa lenye hazina ya wataalamu hao.

Godfrey Sospeter (22) na Neema James (21), wanafunzi wa Taasisi ya Teknolojia Dar-Es-Salaam (DIT), kwa nyakati tofauti wanaonyesha namna elimu waliyoipata inavyoendeleza ubunifu na ugunduzi wao kuelekea kupata suluhisho kwenye matatizo ya jamii hasa sekta ya afya.

Kwenye mahojiano na Nipashe hivi karibuni, wanaeleza namna walivyobuni njia ya kuboresha afya kwa kuunda kifaa cha kupima ...

... wamebaini kuwa kifaa hicho, hakipo kwenye hospitali nyingi nchini zikiwamo yalikofanyika majaribio licha ya kwamba katika nchi zilizoendelea ni muhimu na hutumiwa kwenye hospitali kuupima ubora wa oksjeni kabla ya kumwekea mgonjwa.

"Tunaona kuwa kinahitajika kifaa cha bei nafuu chenye ubora wa hali ya juu kupima ubora wa kiwango cha oksijeni kwa ajili ya wagonjwa wenye mahitaji hayo," anaongeza.

Anasema uwepo wake ndani DIT, umemfanya ajifunze mengi na kufanya ubunifu wa kifaa cha kupimia ubora wa oksijeni inayotumiwa na wagonjwa wodini.

Aidha, kifaa hicho kinaweza pia kupima kiwango na ubora wa oksijeni kwenye mtungi, kabla ya kuwekea mgonjwa wodini, lakini hata eneo alipolazwa pia kufahamu ubora wa hewa anayovuta.

Godfrey anasema kitalaamu oksijeni inayotumiwa huzalishwa kwa njia tofauti na kutaja teknolojia ya kuchuja hewa iliyoko kwenye mazingira watu wanaoishi kupata kiwango kinachohitajika.

Anasema hewa ina gesi za nitrojeni, oksijeni, kaboni na hydorojeni na hivyo huchujwa kupata kiwango cha oksijeni ...

UKURASA 11

Jumanne Februari 14, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581221
www.ippmedia.com
T… …ital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# Vitabu 16 marufuku ukiukaji wa maadili

• **Shule**, taasisi itakayobambwa navyo kukiona... *Endelea Uk.2*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizindua bendera ya mahakama kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Sheria, jana viwanja vya Mahakama Kuu Zanzibar. Kulia ni Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdallah, na (wa tatu kulia) ni Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma. **PICHA: IKULU**

## Makali ya mfumuko wa bei vyakula na vinywaji yapaa zaidi

UKURASA 3

## Benki ya Dunia yasema uchumi wa Tanzania umezidi kuimarika

UKURASA 2

REACH A WIDER AUDIENCE THIS
Valentine
SEASON
AT AN AMAZING OFFER
UP TO 25% Off
On valentine season advertisements*
FROM 10th FEB TO 20th FEB 2023
The Guardian
SUPER BRAND LEADING ENGLISH DAILY
Nipashe
YOUR FAVORITE SWAHILI DAILY
TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON
+255 677 020 701
Email: advertise@guardian.co.tz
Or visit us at Mikocheni light industrial area Opposite ITV / Radio One Dar-es-Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com
*Terms and conditions apply.
Followus: @Theguardiantz



Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdalla (kushoto) na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma (kulia), pamoja na majaji wakuu wa Mahakama Kuu Zanzibar wakiingia katika hafla ya maadhimisho ya Siku ya Sheria Zanzibar jana kwenye viwanja vya Mahakama Kuu Tunguu, Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja. **PICHA: IKULU**

# Vitabu 16 marufuku kwa ukiukaji maadili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof.Adolf Mkenda, ametangaza kupiga marufuku vitabu 16 ambavyo maudhui yake yanakwenda kinyume cha mila, desturi na utamaduni wa kitanzania.

Aidha, amesema shule yoyote itakayobainika kuwa na vitabu hivyo, hatua kali zitachukuliwa ikiwamo kufutiwa usajili.

Akitangaza uamuzi huo jana jijini hapo, Prof. Mkenda alisema vitabu hivyo havipaswi kutumika shuleni na taasisi za elimu kwa kuwa vinakinzana na mila, desturi na utamaduni wa Mtanzania.

"Vitabu hivi vinahatarisha malezi ya watoto na vijana wetu. Vitabu vinanavyopigwa marufuku ambavyo orodha imetolewa ni pamoja na diary of a wimpy kid, diary of a wimpy kid-Rodrick rules, diary of a wimpy kid-the last straw, diary of a wimpy kid-dog days, diary of a wimpy kid-the ugly truth, diary of wimpy kid-cabin fever, diary of a wimpy kid-the third wheel, diary of a wimpy kid-hard luck," alisema.

Alivitaja vingine kuwa ni diary of a wimpy kid-the long haul, diary of wimpy kid-old school, diary of a wimpy kid-double down, diary of wimpy kid-the gateway, diary of wimpy kid-diper overlode, Is for transgender (you know best who you are), Is for LGBTQIA (find the words that make you you) na sex education a guide to life.

Prof. Mkenda alisema vitabu hivyo vikikutwa shuleni, wahusika watakuwa wamevunja sheria na hatua kali zitachukuliwa. Pia aliwahimiza wazazi kukagua mabegi ya shule ya watoto wao ili kuhakikisha havitumiki nyumbani.

"Hii ni orodha ya kwanza ya vitabu baada ya kufanyika ukaguzi na kuhakikiwa na ukaguzi bado unaendelea. Tunahimiza wazazi, walimu, wanafunzi na mtu yeyote atakayegundua kitabu ambacho kinakinzana na maudhui, apige simu kwenye kituo cha huduma kwa mteja kwa namba 02621602270 au 0737 962965," alisema.

Alifafanua kuwa vitabu vya kiada vimehakikiwa na kutumika shuleni na kuna vya ziada ambavyo vimehakikiwa na vinatumika kufundishia.

"Ukiwa na maktaba unakuwa na vitabu vingine zaidi labda novel na vitabu hivi havipo kwenye vitabu vya kufundishia na si vitabu vya kiada au vya ziada ambavyo vimepata ithibati ya kamishna wa elimu nchini vimeingia tu."

"Tumekagua na si kwenye shule zote lakini hivi vichache tukikagua zaidi tutapata na vingine ndio maana tunahimiza tupewe taarifa," alisema.

Waziri Mkenda alisema ziko baadhi ya shule zilizokaguliwa vitabu hivyo vimekutwa katika maktaba zao na kuwataka kutambua vitabu hivyo havitakiwi kwa shule na taasisi ya elimu yoyote iliyopo nchini.


**bgtl BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **NMB BANK PLC** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa wadaiwa waliyetajwa hapo chini, walipe madeni wanayodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) zilizodhamini mikopo yao kwa MNADA WA HADHARA.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAWI | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ABDUL IMANI MGENI | Nyumba ya makazi iliyopo majohe kichangani manispaa ya ilala. | G/MBOTO | 28/02/2023 |
| 2 | JOSEPH NYAMBARI SINDA | Nyumba ya makazi iliyopo majohe mtaa wa kerezange manispaa ya ilala. | G/MBOTO | 28/02/2023 |
| 3 | BENSON NAHUM BAREGE | 1) Nyumba ya makazi yenye kipande cha ardhi na.TMK/MBGL/KZG5/299 yenye leseni no TMK032102 iliyopo kizinga manispaa ya temeke<br>2) Nyumba ya makazi yenye kiwanja no 28&29 kitalu H leseni no.139102 na no.551610 iliyopo chamazi manispaa ya ilala | B/CENTRE | 03/03/2023 |
| 4 | JOSEFINS FIDELIS WILLIAM | Nyumba ya makazi iliyopo kitunda shule manispaa ya ilala | B/HOUSE | 10/03/2023 |
| 5 | MUSSA KIPANJE ZUBERI | Nyumba ya makazi iliyopo mbande mtambani manispaa ya mkuranga | MBAGALA | 17/03/2023 |
| 6 | PLATNUM KUKU | Nyumba ya makazi iliyopo kiharaha kiembeni kata ya mapinga bagamoyo | TEGETA | 24/03/2023 |
| 7 | OJEN SHADRACK JUMA | Nyumba ya makazi iliyopo madale mtaa wa nyakasangwe wilaya ya kinondoni | TEGETA | 24/03/2023 |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**
**Email: info@bestgoup.co.tz**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**NMB Bank PLC,**
**Ohio Street / Ali Hassan Mwinyi Road,**
**P.O. BOX 9213,**
**DAR ES SALAAM**
**Telephone: +255 22 2322550**
**email: Benedicto.Baragomwa@nmbbank.co.tz**

217278302


## Uchumi wa Tanzania wazidi kuimarika

**Na Jenifer Gilla**

LICHA ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID- 19 kuzorotesha uchumi wa nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara, ripoti ya Benki ya Dunia (WB) imeonyesha kuwa uchumi wa Tanzania umezidi kuimarika na kupita wastani wa nchi hizo.

Ripoti hiyo ambayo ni toleo la 18 la Taarifa ya Kiuchumi ya Tanzania, pia imeeleza kwamba pato la Tanzania linatarajia kupanda kutoka asilimia 4.6 mwaka jana hadi asilimia 5.3 mwaka huu.

Sehemu ya ripoti hiyo iliyotolewa jana jijini Dar es Salaam ilitaja sababu zilizochangia kukua kwa uchumi wa Tanzania ni kufunguliwa kwa shughuli za utalii, mipaka kwa shughuli za kiuchumi na mafanikio kwenye chanjo dhidi ya ugonjwa wa corona hali iliyofungua nyanja za biashara na uzalishaji.

Pamoja na mambo mengine ripoti hiyo iliisifu misingi ya kiuchumi ya Tanzania kuhimili misukosuko ya kiuchumi iliyoziumiza nchi nyingi za Afrika kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Ripoti hiyo imeeleza kuwa licha ya ugonjwa wa corona kudhorotesha uchumi wa nchi za Jangwa la Sahara lakini uchumi wa Tanzania umezidi kuimarika.

Pia ilisema kuwa mlipuko wa COVID- 19 ulisababisha kiwango cha umaskini kuongezeka kutoka asilimia 26 mwaka 2019 hadi asilimia 21 mwaka 2021 kwa nchi nyingi za kusini mwa Jangwa la Sahara, ikiwamo Tanzania.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, endapo kusingekuwapo na misingi imara ya kiuchumi, hali ingekuwa mbaya zaidi kutokana na kuwapo kwa uzalishaji mdogo.

Aidha, ripoti hiyo imetaja sababu zilizokwamisha kukua kwa pato la taifa kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa bei za mafuta kulikosababisha usafiri kuwa wa shida, kupanda kwa bei za vyakula kulikosababishwa na kudorora kwa kilimo kutokana na ukame.

Ripoti hiyo pia ilisema upatikanaji wa huduma bora ya maji unaweza kuipunguzia harasa ya kiuchumi Tanzania ya Dola za Marekani bilioni 1.9 (Sh.trilioni 4.48) kwa mwaka ifikapo mwaka 2030.

Tanzania, kwa mujibu wa ripoti hiyo, inaweza kuokoa zaidi ya Dola za Marekani bilioni 2.4 ( Sh. trilioni 5.59) kila mwaka kwa kuepuka gharama za ziada za matibabu zinazopotea kutokana na ukosefu wa uzalishaji na magonjwa yanayotokana na kukosekana kwa huduma hiyo.

Ingawa nchi imepiga hatua kubwa miaka ya hivi karibuni katika kuboresha upatikanaji wa huduma hiyo, ripoti ilibainisha kuwa ni asilimia 61 tu ya kaya ndizo zinazoweza kuipata jambo linaloonyesha bado kuna kazi ya kufanya ili kufikia asilimia 39 iliyobaki.

Akizungumzia ripoti hiyo, Mkurugenzi wa WB Tanzania, Nathan Belete, alisema maji ni huduma ya msingi kwa asilimia 32 ya usafi wa vyoo, huku asilimia 48 ikiwa ni matumizi mengine ya nyumbani ikiwamo kuosha vyombo, kuoga na kufua.

"Ili Tanzania ihakikishe kuna upatikanaji wa majisafi kwa wote, uwekezaji mkubwa wa mapema unahitajika ili kuepuka matokeo mabaya ya huduma duni," alisema Belete.

Alisema moja ya matokeo ya haraka ya zaidi ya huduma duni za majisafi ni vifo na magonjwa lakini uwajibikaji unaweza kuzuia vifo 31,000 vinavyoweza kuzuilika," alisema.

Kadhalika ripoti hiyo inataka kuweka kipaumbele kwenye athari mtambuka zinazotokana na ukosefu wa huduma za majisafi kwenye ajenda kubwa ya sera ya serikali.

Mtaalamu Mwandamizi wa Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa WB, Ruth Walker, alisema utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Sekta ya Maji Tanzania (WSDP III) unahitaji wastani wa Dola za Marekani bilioni 6.5 (Sh. trilioni 15.15).

**HABARI KITAIFA**

# Kortini madai kukutwa na meno ya tembo

**Hadija Kitwana,** KILOMBERO

WAKAZI wawili wa Tarafa ya Mlima, wilayani Kilombero mkoani Morogoro, Julius Ngatunga (55) na Senegal Mtama (27), wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kilombero kwa madai ya kupatikana na meno matatu ya tembo.

Wakati hao wakifikishwa kwa madai hayo, mkazi mwingine wa Mlimba, Noris Gumba, amefikishwa katika mahakama hiyo akikabiliwa na mashtaka sita likiwamo la kukutwa na nyara za serikali pamoja na risasi 18 kinyume cha sheria.

Ngatunga na Mtama walifikishwa mahakamani hapo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Luzango Khamsini na kusomewa shtaka la kupatikana na nyara hizo za serikali.

Akiwasomea shtaka hilo, Mwendesha wa Mashtaka wa Maliasili, Clement Manongi, alidai kuwa Januari 31, 2023 maeneo ya Viwanja 60, Mlimba, washtakiwa walikutwa na meno matatu ya tembo yenye thamani ya Sh. 71,250,000 ambayo ni mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Manongi alidai kuwa upelelezi wa shauri hilo haujakamilika, hivyo washtakiwa hawapaswi kujibu tuhuma hizo hadi pale upelelezi ukikamilika.

Hakimu Khamsini, alisema kutokana na kosa linalowakabili kuwa na thamani kubwa, kila mshtakiwa anatakiwa kuweka hati ya mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni 17 au kuwasilisha fedha yenye thamani hiyo na mdhamini mmoja ambaye atatia saini fungu la dhamana.

Kutokana na washtakiwa hao kutokukidhi masharti ya dhamana, walipelekwa rumande na sharti litatajwa Februari 27, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Mkazi wa Mlimba, Noris Gumba, amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kilombero akikabiliwa na mashtaka sita likiwamo la kukutwa na nyara za serikali pamoja na risasi 18 kinyume cha sheria.

Mshtakiwa huyo alifikishwa jana katika mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Luzango Khamsini.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Francis Malembo, alidai kuwa katika shtaka la kwanza, Januari 30, 2023 katika Kitalu cha Kilombero North Safaris Wilaya ya Kilombero, Gumba alikutwa akiwa na nyama ya nyati pamoja na mkia wa nyati vyote vikiwa na thamani ya Sh. 4,442,200 kinyume cha sheria ya wanyamapori.

**Mshtakiwa huyo alifikishwa jana katika mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Luzango Khamsini.**

Katika shtaka la pili, alidai kuwa tarehe na muda na eneo hilo hilo, mshtakiwa alikutwa na risasi nane za silaha aina ya Rifle 375 bila kibali na katika shtaka la tatu, Malembo alidai kuwa muda na eneo hilo hilo, mshtakiwa alikutwa na risasi mbili za silaha aina ya Shortgun bila kibali.

Katika shtaka la nne, ilidaiwa kuwa mshtakiwa alikutwa na risasi saba za kienyeji za silaha aina ya shotgun bila kibali. Pia katika shtaka la tano, mwendesha mashtaka alidai kuwa mshtakiwa alikutwa na ganda la risasi aina ya rifle 375 bila kibali.

Mwendesha mashtaka huyo alidai kuwa katika shtaka la sita, mshtakiwa muda na eneo hilo hilo, alikutwa na maganda manne ya risasi aina ya shotgun bila kibali.

Malenbo alidai kuwa upelelezi wa shauri hilo haujakamilika, hivyo mshtakiwa haruhusiwi kujibu chochote hadi upelelezi utakapokamilika.

Hakimu Khamsini alimpa masharti ya dhamana mshtakiwa kuwa awe na wadhamini wawili na kutia saini fungu la dhamana la Sh. milioni tano.

Mshtakiwa alipelekwa rumande baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana na kesi imeahirishwa hadi Februari 27, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

# Makali ya mfumuko wa bei za vyakula, vinywaji yaongezeka

**Na Jenifer Gilla**

MFUMUKO wa bei za vyakula na winywaji visivyo na pombe kwa Januari, 2023 umeongezeka hadi asilimia 9.9 kutoka 9.7 iliyorekodiwa Desemba, 2022 na Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS).

Aidha, kiwango cha mfumuko wa bei kwa mwaka kwa bidhaa zote bila chakula na vinywaji visivyo na pombe kwa Januari, 2023 imeongezeka hadi asilimia 3.0 kutoka 2.9 iliyorekodiwa Desemba, 2022.

Kwa mujibu wa NBS, hali hiyo imesababisha mfumuko wa bei wa taifa kwa ujumla kwa mwaka ulioishia Januari, 2023 uongezeke hadi asilimia 4.9 kutoka 4.8 kwa mwaka ulioishia Desemba, 2022.

Baadhi ya bidhaa za vya vyakula zilizoonyesha kuongezeka kwa mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Januari, 2023 ni ngano asilimia 7.7 kutoka sita mwaka ulioishia Desemba 2022, mchele umeongezeka kwa asilimia 2.5 kutoka 2.1 , mahindi asilimia 2.9 kutoka 2.6 huku unga wa mtama ukiongezeka kwa asilimia 3.9 kutoka asilimia moja.

Bidhaa nyingine kwa mujibu wa NBS ni samaki walioongezeka hadi asilimia 4.3 kutoka 4.2, matunda asilimia 5.5 kutoka 1.9, mboga asilimia 5.2 kutoka 3.6, viazi vitamu asilimia 5.3 kutoka 3.9, choroko asilimia 5.6 kutoka 1.3 na kunde asilimia 13.9 kutoka 8.7.

Aidha, taarifa hiyo imeonyesha kuwa bidhaa zisizo za vyakula nazo zimeongezeka bei ukilinganisha na mwaka ulioishia Desemba 2022.

Baadhi ya bidhaa hizo ni nguo za wanawake zilizoongezeka kwa asilimia 2.7 mwaka ulioishia Januari, 2023 kutoka asilimia 2.6 mwaka ulioishia Desemba, 2022.

Vifaa muhimu kwa matumizi ya nyumbani navyo vilipanda bei kwa asilimia 3.5 kutoka 2.2 mwaka ulioishia Desemba 2022 ni petroli iliyopanda kwa asilimia 4.7 kutoka 2.7, ada za shule kwa asilimia 2.9 kutoka 0.7 na huduma za malazi kwenye hoteli na nyumba za kulala wageni kwa asilimia 3.8 kutoka 0.9.

**WANANCHI WAFUNGUKA**

Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam wamelalamika kuwa kuendelea kupanda kwa bei kunaathiri hali ya maisha ikizingatiwa kuwa vipato vyao havijaongezeka na kujikuta wanatumia fedha nyingi kugharamia vyakula.

Rose James, mkazi wa Kunduchi, alisema kupanda kwa bei ya vyakula hivyo muhimu kila kukicha, kunamrudisha nyuma kimaendeleo kwa kuwa fedha nyingi zinatumika kununua chakula.

"Mimi ni mama wa watoto watatu, ni mfanyakazi. Kwa miaka miwili vyakula vinapanda lakini mshahara uko pale pale. Najikuta kwa sasa natumia asilimia 30 ya mashahara kwenye chakula tu wakati hapo mwanzo nilikuwa natumia asilimia 15. Nilikuwa na ujenzi ila nimeusimamisha kwa kuwa pesa haitoshi," alisema.

Naye Rahid Abdalla, muuza nguo za mtumba katika soko la Karume, alisema hali hiyo imemlazimu kula milo miwili kwa siku baada ya wauza vyakula maarufu kama mama ntilie, kupandisha bei ya bidhaa hiyo.

"Zamani sahani ya wali na nyama ilikuwa inauza hadi Sh.1,000 lakini sasa hivi ili ule ushibe inakulazimu ununue kipimo cha Sh.2,500. Kutokana na hali hiyo nikishakunywa chai saa tano, nakula tena saa 12:00 jioni, siku inakuwa imeisha," alisema.

Mfanyabiashara wa nafaka kwa bei ya jumla katika soko la Temeke, Sheikh Mbwana, alisema kupaa kwa bei ya bidhaa kumesababishwa na upungufu katika mashamba kutokana na kutonyesha kwa mvua za kutosha mwaka jana.

Aidha, alisema kitendo cha serikali kuruhusu wafanyabiashara wa nje ya nchi kununua bidhaa hizo moja kwa moja kwa wakulima, pia kinachangia kupanda kwa nafaka kwa sababu wanalipa kwa fedha za kigeni ambazo ziko juu, hivyo wakulima kuwataka wazawa kununua kwa bei hiyo pia.


## UBALOZI WA MAREKANI DAR ES SALAAM

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **Ubalozi wa Marekani,** watauza kwa mnada wa hadhara Fanicha, Magari na Genereta tarehe 18 February, 2023 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Fanicha na computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi:** Sofa set, Occasional sofa, Dresser, Office Desk, Hutch, Chair, Office partitions, Book Shelve, Book case, Carpet, Vitanda, Magodoro, Garden table/Chairs, Fridge, Freezer, Washer, A/c split units, Printer, Desk Computer, Laptop, TV set, Xerox photo copy model 7855, Spea mpya za Kyocera photocopy, Professional high pressure car wash m/c na vingine vingi.

**Magari, Genereta yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Toyota L. Cruiser GX- V8 Manual Tran. | 1VDO27 Diesel Engine | 2014 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota L.Cruiser GX- V8 Auto Tran. | 1VDO27 Diesel Engine | 2011 | Haujalipwa |
| 2 | Genereta KVA 65 na 32 Phase 3 | Cummins Diesel Engine | - | Haujalipwa |
| 1 | Water Storage Tank | Fiber 90,000 Litters | - | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 15 mpaka 17 February 2023, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari na genereta atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 23 February, 2023 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Genereta litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya **VISA na Master cards za CRDB na NBC** yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini na kuvaa barakoa.
7. Kila mtu anayesiriki mnada ni lazima kuvaa Barakoa na kunawa na maji tiririka au Sanitaiza.

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926** **E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

217278702

# Kigogo CHADEMA atoa neno kuhusu kikokotoo

Na Christina Mwakangale

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Heche (pichani), amesema mfumo wa sasa wa malipo ya mafao kwa wastaafu kwa kutumia kanuni ya kikokotoo kipya, unapunguza mwamko wa uwajibikaji.

Amesema serikali itoe fursa kwa wanufaika wa mifuko ya hifadhi ya jamii na binafsi na umma, kwa kuchagua kupokea mafao ya muda mrefu kwa mkupuo au la, kulingana na mahitaji ya kila mmoja.

Wakati Heche akisema hayo, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Tumaini Nyamhokya, aliiambia Nipashe jana kwamba, kiwango cha kikokotoo kilichopangwa kinaendana na hali na uwezo wa mifuko ya hifadhi ya jamii.

"Mifuko ni yetu sisi wafanyakazi si ya serikali, tunataka tusiwe na viwango visivyoendana na mifuko, kwa wastaafu wa sasa na wajao. Tucta haifanyii kazi maoni ya mtu mmoja kwa hiyo kisiasa hatuwezi kuwaangalia. Asilimia 33 ni kiwango cha manufaa kwa wote," alisema Nyamhokya.

Kabla ya hatua hiyo, wastaafu walilipwa asilimia 50 wanapostaafu na mabadiliko ya kanuni ya kikokotoo ya mafao ya mwaka 2018 ilipendekeza kiwango cha hadi asilimia 25 hatua iliyozua mjadala mkali hadi kufikia uamuzi wa kutoa mafao kwa asilimia 33 ya fedha ya kiinua mgongo.



Akizungumza juzi, Heche alisema malipo makubwa ya mafao kwa mwanasiasa akistaafu ni takribani Sh. milioni 272 huku mtumishi wa umma akilipwa Sh. milioni 47 kiasi ambacho alisema hakiendani na umuhimu wa watu hao kwenye utumishi wa umma.

"Mafao ya mkupuo yanapunguzwa ila ya mwezi yaongezwe. Wako waliokopa magari, nyumba na vitu, hivyo ili aje alipe akipata fedha hiyo ya mafao, mtu amechangia miaka 15 na ametoa Sh. milioni 97 analipwa Sh. milioni 47 nyingine imepotea.

"Kikokotoo kipya analipwa miaka 12 na nusu napo kwa mafungu. Kuna askari mstaafu amesema alichangia kwa miaka 13 na ameenda haoni fedha ya usafiri. Mbunge akilipwa kiinua mgongo kizuri, lakini awe amekifanyia kazi basi sio kupasha kiti moto tu.

"Halafu baada ya miaka mitano, unalipwa fedha nyingi na walimu wetu, askari wanaotulinda, madaktari na watumishi wengine wa umma wanalipwa vibaya," alisema.

"Hii itapunguza uaminifu, watu walioko kazini wanaona jinsi wastaafu wanachopitia. Mtu ili ajiendae ni kwa kuweka akiba ajiandae na kustaafu lakini sasa wataanza kutafuta fedha ya kustaafu sasa. Serikali ibadilishe msimamo katika hili, isivunje makubaliano baina ya serikali, mifuko na wafanyakazi," aliongeza.

Alisema serikali inapaswa kufanya utafiti kubaini sababu ya mifuko hiyo kufilisika, huku fedha zikichangwa na wanachama wa mifuko hiyo kila mwezi.

Msemaji wa Sekta ya Uwekezaji, Mashirika ya Umma na Hifadhi ya Jamii wa Chama cha ACT-Wazalendo, Mwanaisha Mndeme, alisema hatua ya serikali kutotumia kanuni mpya ya kikokotoo baada ya mjadala wa miaka mitatu na mapendekezo mbalimbali ya kuboresha maslahi ya watumishi ni kupuuza sauti za wanyonge.

"Ni dhahiri kuwa serikali imeamua kupuuza sauti za muda mrefu za wafanyakazi na kuonyesha kuwa lengo lake ni kuwaumiza wastaafu. Ujio wa kanuni hizi, kwa kumlipa mstaafu asilimia 33 ya mafao ya mkupuo, kwa miaka 12.5 na kikokotoo cha 1/580 ni kuwakandamiza na kuwanyonya.

"Mazingira magumu ya mishahara kiduchu, ambayo inayowafanya kuishi kwenye mzunguko wa madeni kila uchao. Ni wazi kuwa kanuni hizi zitashusha ari, hamasa na ufanisi wa kazi kwa wafanyakazi wa nchi hii," alisema.

Baadhi ya watu walitoa maoni yao kuhusu suala hilo kwenye mitandao ya kijamii, John Jackson alisema: "Umenena vyema kabisa, mtu anafanya kazi miaka 30 au zaidi kiinua mgongo Sh. milioni 60 tena sasa wameleta kikokotoo anapata milioni 20. Hivi hii haki kweli?"

Matatizo Lukuki alisema : "Kikokotoo hiki kipya kimeanza kufanya kazi mwaka huu wa fedha yaani 2022/23 ambapo mtumishi akistaafu analipwa asilimia 33 kama mkupuo. Usiombe yakukute au yamkute wa karibu yako."

# Wataalamu wa afya wanolewa kukabili magonjwa ya dharura

Beatrice Moses

WATAALAMU 150 wa masuala ya afya kutoka mikoa tofauti nchini, wameingizwa kwenye mafunzo maalum ya kimataifa ya kupambana na kutoa huduma za tiba yanapozuka majanga na magonjwa ya dharura.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Huduma za Tiba kutoka Wizara ya Afya, Prof. Pascal Ruggajo, alisema yameandaliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) yanatolewa kwa mwezi mmoja.

Prof. Ruggajo aliyemwakilisha mgeni rasmi, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa kuwa yanahusisha wataalamu wa afya kutoka maeneo tofauti yakiwamo kilimo na lishe, ustawi wa jamii, madaktari na wauguzi wa afya ya binadamu na wanyama.

"Janga la UVIKO -19 lililoibuka katika nchi mbalimbali duniani, lilitoa funzo kwa Tanzania kwa hiyo matunzo haya ni muhimu kwa kuwa yanaandaa timu maalum ambayo itatumika wakati wowote katika kutoa elimu au kupambana na janga la ugonjwa litakaloibuka," alisema Prof. Ruggajo.

Alisema kuwa mafunzo hayo yana umuhimu kwa kuwa yameunganisha sekta zinazohusiana na afya kwani baadhi ya magonjwa ya milipuko hutoka kwa wanyama au mazao hivyo ni inapaswa kuwa makini kwa pande zote hizo ili kushirikiana kutatua changamoto zinazoweza kuibuka kwa magonjwa ya dharura.

Kaimu Mwakilishi wa WHO Tanzania, Dk. Zabulon Yoti, aliipongeza serikali ya Tanzania kwa kufikia hatua hiyo muhimu ya kujenga uwezo wa nchi kujiandaa, kugundua na kukabiliana na dharura za kiafya.

Alisema dunia inakabiliwa na aina mbalimbali za hatari zinazohusishwa na dharura za kiafya, hivyo nchi zote ikiwamo Tanzania ziko hatarini.

"Tathmini ya hivi karibuni ya hatari ya kimkakati iliyofanywa Septemba, 2022 ilionyesha kuwa nchi kadhaa za Afrika ziko katika hatari kubwa ya kuzuka kwa magonjwa ya kuambukiza," alisema.

Dk. Yoti alisema dharura za kiafya haziogopi wala kuheshimu mipaka ya kitaifa, hali hiyo imeonekana mara baada ya kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza.

"Nataka kusisitiza kwamba dharura za kiafya pia haziheshimu mipaka ya taaluma zetu duniani kote. Karibu magonjwa matatu kati ya manne 4 mapya au yanayoibuka ya kuambukiza kwa watu hutoka kwa wanyama," alisema.

Alisema kati ya matukio 2,000 au zaidi ya afya ya umma yaliyorekodiwa katika eneo la Afrika katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, inakadiriwa kuwa zaidi ya nusu ya matukio yanahusiana na hali ya hewa.


Summons to an Accused Person (S.19)
Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 16 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

ALEX MATOVU

To:

Alex Matovu
Container Area, Wazo Ward
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 02 day of MARCH 2023 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JANUARY 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me:

Name……………………………

Signature……………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………

Summons to an Accused Person (S.19)
Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 14 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

BARTON HAMIS MWASAMENGO

To:

Barton Hamis Mwasamengo
Plot No. 1046, Block G
Mbezi Luis Area,
Ubungo Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 02 day of MARCH 2023 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me:

Name……………………………

Signature……………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………

217278102

## HABARI KITAIFA

# Gavana afurahia mabadiliko dijitali sekta ya kifedha

**Na Joseph Mwendapole**

GAVANA wa Benki Kuu Tanzania (BOT), Emmanuel Tutuba, amepongeza mabadiliko ya kidijitali kwa sekta ya kibenki katika kuimarisha ujumuishaji wa fedha nchini.

Aliyasema hayo juzi jioni wakati akizungumza katika hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na wanachama wa Chama cha Benki Tanzania (TBA), jijini Dar es Salaam.

Hafla hiyo ilikuwa maalum kwa ajili ya kumkaribisha Gavana Tutuba, aliyeteuliwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan na kumuaga aliyekuwa Gavana, Prof. Frolence Luoga, ambaye amestaafu.

Gavana Tutuba alipongeza safari ya mabadiliko ya kidijitali ambayo benki za biashara zimeanza katika kutoa urahisi na kufikia wigo mpana wa wateja.

"Utendaji imara wa benki katika mwaka uliopita ni ushuhuda wa mawazo ya kibunifu yaliyowekwa na benki kuvutia wateja zaidi na kuwapa uzoefu bora. Serikali inatambua kazi nzuri ambayo benki hizo zimekuwa zikifanya katika kupanua huduma za kifedha kwa Watanzania walio wengi, wakiwamo katika sekta rasmi ya fedha."

"Naipongeza TBA kwa jitihada zake mbalimbali kwa miaka mingi na nazipongeza benki kwa utendaji wao mzuri wa kifedha na BoT inaahidi kuendelea kushirikiana," alisema Gavana.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chama cha Benki Tanzania (TBA), Theobald Sabi, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara ya Taifa (NBC), aliishukuru serikali na BoT kwa ushirikiano na jitihada endelevu katika kukuza mazingira mazuri ya kibiashara.

"TBA inatambua ushirikiano na msaada kutoka serikalini na BoT ambao umesababisha sekta ya fedha kupiga hatua kubwa. Kwa mfano, kufikia Desemba 2022, Benki za Tanzania zilipata faida ya zaidi ya Sh. trilioni 1.164, ikiwa ni mara ya kwanza katika historia," alisema.

"Tumeona pia ukuaji mkubwa katika maeneo mengine, kama vile huduma za kibenki kupitia mawakala, kidijitali, mikopo kwa sekta binafsi na miongozo ya biashara yenye kujenga ambayo imetufanya kustawi tunashukuru sana," alisema Sabi.

Mkurugenzi Mtendaji wa TBA, Tusekelege Joune, alisema TBA kwa sasa inatekeleza mkakati wa miaka mitano (2023-2027) ambao utazinduliwa hivi karibuni kwa umma.

"Nina furaha kutangaza kwamba mpango wetu wa miaka mitano sasa uko tayari kwa uzinduzi na hivi karibuni tutaupeleka kwa umma," alisema.

TBA ni chombo cha utetezi cha wanachama kwa sekta ya benki ambacho kinajitahidi kuleta wanachama pamoja kupitia ushirikiano hususani ushirikiano wenye maslahi ya pamoja.

# Tanzania yaongoza uzalishaji mikunde

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

TANZANIA imetajwa kuwa mzalishaji bora wa mazao ya mikunde Afrika Mashariki na mwaka 2021 ilikadiriwa tani milioni 1.8 zilizalishwa na kuuzwa nje ya nchi kwa dola za Marekani milioni 266 mwaka 2023 kutoka milioni 198 mwaka 2020.

Ofisa Lishe wa Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), Stella Kimambo, alisema hayo juzi katika maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Mikunde, kwa niaba ya Mwakilishi Mkazi wa shirika hilo, Dk. Nyabenyi Tipo.

Alisema asilimia 85 ya mauzo ya mazao hayo yamekua yakisafirishwa kwenda nchini india.

"Pamoja na umuhimu wake kwa lishe, mwenendo wa ulaji wa mikunde nchini Tanzania umekua ukipungua mara kwa mara. Familia nyingi zimechukulia mazao ya mikunde kama chakula cha watu maskini, hivyo kupunguza ulaji wake katika meza zetu pale nyama inapoonekana inanyanyapaliwa. Watu wengi hula maharage lakini mbaazi, dengu na choroko havipati nafasi," alisema Kimambo.

Kutokana na hali hiyo, Kimambo aliomba serikali kuweka makubaliano ya kibiashara na India, ili kufanikisha na kuhakikisha nafasi ya kiupendeleo unakuwepo katika soko la mikunde duniani.

"Tunaomba pia kwa mipangilio ya kitaasisi kuhamasisha matumaini ya ndani ya mikunde kupitia programu ya chakula shuleni, gerezani, jeshini ili kujengea uwezo soko la ndani la mikunde sio kutegemea pia masoko ya nje kama vile soko kubwa moja la India.

"Tunapendekeza matumizi ya kawaida katika ngazi ya kaya, hotel na kutoa fursa katika vyombo vya habari zao la mikunde liweze kuhamasishwa kwa nguvu," alisema Kimambo.

Ofisa Kilimo wa Wizara ya Kilimo, Magreth Natai, alisema wanatekeleza mradi wa Agri-Connect ili kuhamasisha na kujenga utamaduni wa kula vyakula aina ya mikunde.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema uzalishaji wa mazao ya mikunde nchini bado ni mdogo ili kufikia soko la kimataifa.

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)**

**CRIMINAL CASE NO.** 19 **OF** 2023

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**ALBINA MASSAWE AS GUADIAN OF JOEL & MATILDA MAGOTO**

**To:**

Albina Massawe *(As Guardian of Joel & Matilda Magoto)*
Mivumoni Area, Kawe Ward
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 02 day of MARCH 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN 2023

**RESIDENT MAGISTRATE**

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name………………………………

Signature………………………………

Qualification/Relationship

Date………………………………

217278102

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM** ***(AT KINONDONI)***

**CRIMINAL CASE NO.** 52 **OF** 2023

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**DARPCO ENERGY CO. LIMITED**

**To:**

The Filling Station Manager
Darco Energy Co. Limited
Kunduchi Filling Station
Mtongani Street, Kunduchi Area
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 3rd day of MARCH 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27TH day of JAN. 2023

**RESIDENT MAGISTRATE**

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name………………………………

Signature………………………………

Qualification/Relationship

Date………………………………

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM** ***(AT KINONDONI)***

**CRIMINAL CASE NO.** 52 **OF** 2023

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**DARPCO ENERGY CO. LIMITED**

**To:**

Thabiti Mkasi (0715 345 332)
Managing Director
Darco Energy Co. Limited
Mtongani Street, Kunduchi Area
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 3rd day of March 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27th day of January 2023

**RESIDENT MAGISTRATE**

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name………………………………

Signature………………………………

Qualification/Relationship

Date………………………………

217278102

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)**

**CRIMINAL CASE NO.** 21 **OF** 2023

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**SUBIRA YONA MSUZI**

**To:**

Subira Yona Msuzi
Ukwamani Area, Kawe
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 02 day of MARCH 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN 2023

**RESIDENT MAGISTRATE**

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name………………………………

Signature………………………………

Qualification/Relationship

Date………………………………

217278102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali iende mbali zaidi kufungia vitabu

**SERIKALI** kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, jana ilitangaza kuvipiga marufuku vitabu 16 vya ziada ambavyo maudhui yake yanakiuka mila, desturi na utamaduni wa kitanzania.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, akitangaza uamuzi huo jana jijini Dodoma mbele ya waandishi wa habari, alisema hiyo ni hatua ya kwanza iliyochukuliwa na serikali katika kupambana na uvunjifu wa maadili ya Kitanzania kupitia vitabu hivyo. Alibainisha kwamba ukaguzi zaidi ili kubaini vitabu vyenye mwelekeo huo, unaendelea na kuonya kuwa shule yoyote itakayobainika kuwa na vitabu vya aina hiyo, itakumbwa na adhabu kali ikiwamo kufutiwa usajili.

Pamoja na kutangaza kuchukuliwa kwa hatua hiyo, Waziri Mkenda aliweka bayana kuwa vitabu hivyo havipaswi kutumika shuleni na taasisi za elimu na kwamba vitabu hivyo vikikutwa shuleni, wahusika watakuwa wamevunja sheria na hatua kali zitachukuliwa.

Sambamba na hatua hiyo, Mkenda aliwahimiza wazazi kukagua mabegi ya shule ya watoto ili kuhakikisha havitumiki nyumbani huku akitaka wazazi, walimu, wanafunzi na mtu yeyote atakayegundua kitabu ambacho kinakinzana na maudhui, atoe taarifa katika mamlaka husika au kupiga simu kwenye kituo cha huduma kwa mteja cha wizara kwa namba 02621602270 au 0737 962965.

Kwa mujibu wa Waziri Mkenda, vitabu hivyo vimegundulika baada ya ukaguzi uliofanyika katika shule mbalimbali na kukutwa vikitumika kama vitabu vya ziada katika maktaba za shule husika.

Hatua iliyochukuliwa na serikali kwa ujumla ni ya kupongezwa kwa kuwa ina lengo mahususi la kulinda mila, utamaduni na desturi za Kitanzania ambazo kwa kiasi kikubwa zimeathiriwa na ujio wa utandawazi na soko huria.

Kuwapo kwa mfumo huo kumesababisha kuingizwa kwa bidhaa mbalimbali hata zile zisizoruhusiwa kwa mujibu wa mila na utamaduni wa kitanzania na kiafrika na matokeo yake, vijana wengi wameharibiwa. Hivi sasa kuna vitendo vya ushoga na hamasa za mapenzi ya jinsia moja ndani ya shule na taasisi za elimu ambavyo mwelekeo wake ni kuharibu maadili mema ya Kitanzania.

Kama wahenga wasemavyo mzaha mazaha mwisho hutumbuka usaha, kuendelea kuacha mambo hayo yaendelee, ni kuliangamiza taifa kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kushamiri wa ushoga na ndoa za jinsia moja, ambazo zinashadadiwa na mataifa ya nje kwa rubuni za misaada na mambo mbalimbali.

Licha ya kupongeza hatua hiyo, swali linabaki ni kwa namna gani vitabu hivi vilipenya hadi kuingia nchini na kuanza kutumika katika shule kama vitabu vya ziada? Ni dhahiri kwamba kulikuwa na ulegevu mahali au baadhi ya maofisa waliopewa dhamana ya kudhibiti ubora wa elimu kukengeuka ikiwamo kupewa rushwa na kusababisha 'matundu' hayo katika elimu.

Wahenga wanasema yaliyopita si ndwele tugange yajayo, hivyo hakuna budi kusahau au kuanza kushikana uchawi juu ya nani au kikundi cha watu gani kilichoruhusu kuwapo kwa uvunjifu wa maadili kupitia vitabu hivyo, bali mkazo uwe katika kufanya ukaguzi zaidi ili kubaini vitabu vingine zaidi.

Sambamba na hilo, ni vyema serikali ikaenda mbali zaidi kwa kukagua hata mikanda ya video inayoingizwa au kutengenezwa nchini ambayo inakiuka mila na desturi za Kitanzania. Ili kutimiza hilo, ukaguzi ufanyike katika maduka yanayouza mikanda hiyo pamoja na vibanda 'umiza' vinavyoonyesha picha za video hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Mwandishi Wetu

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni siku ya upendo si ya kujamiiana

**LEO** ni siku ya kuonyesha upendo kwa mwenza, wazazi, watoto, ndugu na marafiki. Ni Sikukuu ya Wapendano ya 'Valentine's Day'.

Hata hivyo, mwanasaikolojia Sadaka Gandi, anapoitazama anatoa angalizo kuwa imepotoshwa na kutaka mabadiliko.

Siku hii ya wapendanao huadhimishwa kila Februari 14, dunia kote, historia yake huanzia karne ya tatu huko Roma au Terni ikianzishwa na Askofu Valentinus, ambaye Wakatoliki wanamheshimu kama mtakatifu.

Kwa mujibu wa historia, Kaisari au Mtawala wa Warumi, kipindi hicho alikuwa Claudius II ambaye aliweka sheria kwa askari wote wasioe wala kufungua ndoa, akiamini ukakamavu upo kwa makapera sio kwa wanandoa.

Padri Valentinus alipinga sheria hiyo na kuendelea kufungisha ndoa kwa siri akiamini katika makusudio ya kupinga zinaa. Mfalme Claudius II alipata taarifa na kuamuru akamatwe na anyongwe.

Akiwa gerezani kusubiri hukumu ya kifo chake, aliandika barua ambayo ilikuwa na salamu za kwanza za Valentine kwa binti aliyekuja kumsalimia gerezani mwisho wa barua hiyo alihitimisha kwa maneno kutoka kwa 'Valentine wako".

Toka hapo Valentinus anakumbukwa kama mtetezi wa wapendanao na sikukuu yake kuadhimishwa karibia duniani kote.

Warumi ni siku ya kumbukumbu na sehemu nyingine ni 'festum' ikimaanisha siku ya daraja la kwanza kwa kumkumbuka Padri Valentine aliyeuawa na utawala wa Kirumi sababu ya kutetea waumini wake kufunga ndoa badala ya mume na mke kuishi pamoja bila ndoa.

Lakini, sikukuu hiyo imeenea sana katika nchi za magharibi na baadaye karibia sehemu kubwa ya dunia na kuisherehekea kama siku ya wapendanao kinyume cha dhamira ya Mtakatifu Valentinus.

Kwa miaka ya hivi karibuni maudhui ya siku hiyo imechukua maana ingine ya kupotosha ikitawaliwa na vitendo vya ngono hasa kwa wasio wanandoa ili mradi wanapendana, kitu ambacho ni kinyume cha malengo ya Mtakatifu Valentinus aliyetaka vijana wafunge ndoa badala ya kuwa na uhusiano usio na maadili kwa binadamu na kwa Muumba wao.

Sadaka anasema, haungi mkono siku hiyo kwa sababu imekuwa chanzo cha mambo mabaya, akidhani mkanganyiko wa makusudio ya awali na sasa ni tofauti ndiyo sababu ya ndoa nyingi kuvunjika.

Anasema maana halisi ya upendo imefifia na kuwaacha watu wengi kuwa katika msongo wa mawazo hiyo inayoleta ongezeko kubwa la wanawake na wanaume walioumizwa na wenza.

Nami naungana na Sadaka kueleza kuwa Sikukuu ya Wapendao imekuwa ndiyo wakati wa watu kutoka na kuchukua waume wa watu.

Ni wakati wanaume wasio na maadili wanawaharibia mipango ya kitaaluma watoto wa shule wanawapa zawadi nyingine za kila namna kisa ni kuwawatumia kingono.

Zawadi mbaya zaidi wanazobaki nazo mabinti ni mimba za utotoni, maradhi kuanzia saratani ya kizazi, ukeni na sehemu ya haja kubwa inayoambukizwa na virusi vya HPV vinavyofikishwa kwenye maeneo ya uzazi au sehemu zote za haja kupitia kujamiiana.

Mara nyingi HPV huishi kwenye maeneo ya siri ya wanaume. Kuendelea 'kupendana' kwa misingi ambayo hailingani na malengo ya Mtakatifu Valentunus, kumeongeza matatizo kwenye jamii, mojawapo ni watu wengi kuangukia katika magonjwa ya afya ya akili, ndoa kuvunjika, mabinti kukatisha masomo, sonona lakini kuongezeka watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu baada ya wazazi kuachana.

Sadaka anasema anaikataa Valentines' Day kwa sababu imekuwa chanzo cha ndoa kutetereka na mahusiano kuyumba, imejenga matarajio makubwa ambayo yamesababisha kusumbua akili za wengi na hivyo kusababisha maumivu yaliyo limbikizwa na hivyo kupelekea ndoa nyingi kuvunjika na vijana kuingia katika uhusiano na vitendo vya ngono wakidai kusherehekea siku hiyo.

Ni wakati wa kuamka na kuitumia siku hiyo kutambua umuhimu wakufahamu mambo yanayovuruga uhusiano wako, hasara za kuvunja ndoa, kujamiiana na mabinti au watu wazima bila kujali hatima yako.

Ni vyema kutafakari upya uhusiano wako na kuanza kuishi katika ukamilifu badala ya kujihalalishia kuwa Februari 14 ni siku ya kufanya uhalifu kwa kisingizio cha siku ya upendo.

# MV. Mwanza kufungua milango ya uwekezaji

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MELI kubwa zaidi ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu imeshushwa rasmi kwenye maji ikiwa ni ukamilishwaji wa hatua ya pili ya ujenzi wake, huku ikitarajiwa kufungua milango ya uwekezaji nchini pamoja na masoko mapya ya ndani na nje ya nchi.

Inaelezwa kukamilika kwa hatua hiyo ya pili kwa asilimia 100 kunafikisha ujenzi wa meli hiyo katika asilimia 82 kuelekea kukamilika kwake Agosti mwaka huu na kuanza safari zake katika bandari zote kuu zilizoko Ziwa Victoria katika nchini za Uganda, Kenya na Tanzania.

Akizungumza katika hafla hiyo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchunguzi, Atupele Mwakibete, alitoa maelekezo kwa Mamlaka ya Usimamzii wa Bandari Tanzania (TPA) kuhakikisha inasimamia na kukarabati bandari zote kubwa zinazotarajiwa kupokea meli hiyo na zikamilike ndani ya miezi michache.

Alisema lengo ni kuipa nafasi meli hiyo kuzifikia bandari hizo katika usafiri na usafirishaji wa mizigo, ikiwa ni sehemu ya kukuza biashara na uchumi wa nchi.

Pia alisema meli hiyo itafungua milango ya uwekezaji kupitia bandari za Bukoba, Kemondo, Jinja ya nchini Uganda, Portbell ya nchini Uganda, Kisumo ya nchini Kenya pamoja na Musoma.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), Erick Hamisi, alisema meli imegharimu Sh. bilioni 109.1 na tayari mkandarasi amelipwa asilimia 88 ya fedha sawa na Sh. bilioni 93.8, hivyo ikikamilika atapatiwa fedha yote iliyobaki.

Awali, Mkuu wa Mkoa Mwanza, Adam Malima, alisema kukamilika kwa meli hiyo kunatarajia kuongeza nguvu katika usafirishaji wa mizigo na abiria katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya mikoa na nchi.

Malima alisema uwapo wa meli hiyo utakuwa na muunganiko wa karibu na reli ya kisasa ya SGR kwa kupokea mizigo ya treni hiyo inayotokea katika Bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi jirani ikiwamo Uganda.

Alisema nje ya mradi huo bado mkoa wa Mwanza umekuwa mnufaika mkubwa wa miradi mitatu ya serikali ambayo itasaidia katika kuinua uchumi wa mkoa ambayo ni pamoja na reli ya kisasa ya SGR itakayokuwa na bandari kavu inayojengwa Fera, uwanja wa ndege pamoja na meli hiyo kubwa zaidi kuwahi kujengwa katika nchi za maziwa makuu.

Baadhi ya wakuu wa mikoa jirani na wanufaika wa meli hiyo kubwa, walieleza namna mradi huo utakavyonufaisha nchi kwa kuongeza shughuli za uwekezaji.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alisema meli hiyo itakuwa faraja kubwa katika usafirishaji mkoani Kagera hususani kwa wakazi wa maeneo ya visiwani na biashara nyingi zinaendelea na kutegemea bidhaa mbalimbali kutoka katika Bandari ya Dar es Salaam na bidhaa zingine kutoka Uganda.

Vilevile, alisema tayari serikali imetenga Sh. milioni 30 kwa ajili ya ukarabati wa Bandari ya Kemondo ambayo inatarajiwa kupokea meli hiyo kubwa.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella, alisema kupitia uwepo wa meli kutasaidia kuongeza shughuli za uwekezaji hivyo kuwataka wawekezaji kutumia fursa hiyo kuhakikisha wanafanya biashara na uwekezaji mkubwa mkoani humo.




Mkuu wa Mkoa wa Mara, Meja Jenerali Suleiman Mzee, aliiomba serikali kuboresha bandari hiyo ili kupata sehemu ya meli hiyo kuona ikianza safari zake.

Mhandisi Kiongozi wa Mradi wa Ujenzi wa MV. Mwanza Hapa Kazi Tu, Vitus Mapunda, alisema meli hiyo itakapoanza safari zake, itazingatia vigezo vyote vya utunzaji wa mazingira katika eneo la usafirishaji wake.

Meli hiyo yenye uzito wa tani 3,500 itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200, mizigo tani 400 pamoja na magari 20 na kusafiri katika bandari zote kubwa za Ziwa Victoria katika nchini tatu za Afrika Mashariki za Kenya, Uganda na Tanzania.

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 23 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

WILFRED OFORO MARO

To:

Wilfred Oforo Maro
Plot No. 200, Block 42, Kinondoni B
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 02 day of MARCH 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name……………………

Signature……………………

Qualification/Relationship

Date……………………

217278102

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 17 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

FAIZA HASSAN

To:

Faiza Hassan
Plot No. 244, Block 3
Mwananyamala Area, Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 02 day of MARCH 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name……………………

Signature……………………

Qualification/Relationship

Date……………………

217278102

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 25 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

JACQUILINE B. ADOKO

To:

Jacquiline B. Adoko
Plot No. 359, Block 5, Mbezi Beach Area,
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 02 day of MARCH 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name……………………

Signature……………………

Qualification/Relationship

Date……………………

217278102

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 24 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

SIRI AMBROSE MALAI

To:

Siri Ambrose Malai
Plot No. 541, Block E, Sinza Area,
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 02 day of MARCH 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name……………………

Signature……………………

Qualification/Relationship

Date……………………

217278102

# Serikali yageukia uendelezaji zao la mpira

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amesema serikali sasa inaweka mkazo katika uendelezaji wa zao la mpira ambalo lilikuwa halitiliwi maanani miaka iliyopita.

Kutokana na msisitizo huo, amewataka wakulima walioko katika maeneo yenye hali ya hewa kama ya Mang'ula, Kilombero mkoani Morogoro, kulima zao hilo ili kukidhi mahitaji ya soko la asilimia 99.7 ambalo kwa sasa mauzo yake ni asilimia 0.03.

Waziri Kijaji aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita, alipotembelea shamba la mpira la Kalunga lililoko Kata ya Mang'ula, Kilombero mkoani Morogoro kuangalia jitihada zinazofanywa na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) katika kuendeleza uzalishaji wa zao hilo ambalo ni la kimkakati linalotumika kutengeneza bidhaa kama matairi, magodoro na glovu.

Dk. Kijaji pia aliitaka NDC kuelimisha umma kuhusu uzalishaji wa zao hilo huku akitaka Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) na Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo (TEMDO) kutengeneza mashine zitakazowawezesha wakulima kuchakata mpira kwa gharama nafuu ili kufikia malengo ya serikali katika ujenzi wa uchumi jumuishi wa viwanda.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, alisema NDC imeweka utaratibu wa kuondoa miti ya zamani iliyopandwa wakati wa serikali ya awamu ya kwanza mwaka 1978 na imeisha muda wake na kupanda mpya.

Kwa kufanya hivyo, alisema itahakikisha miti hiyo inatoa faida iliyokusudiwa ya mpira, mbao, kuni na utunzaji wa mazingira kwa utoaji wa hewa ya ukaa.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa NDC, Dk. Nicolaus Shombe, alisema shirika hilo limejipanga kuzalisha miche 200,000 ya mpira na inakamilisha taratibu za kuthibitishwa kuwa mzalishaji na msambazaji wa mbegu za mpira ili kuhamasisha wananchi kulima zao hilo na kukidhi mahitaji makubwa ya soko ndani na nje ya nchi.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Christopher Wangwe, aliahidi kuongeza eneo la shamba la Kalunga kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mlimba.

Pia alisema wamepanga kila shule kupanda miche 50 na kila mwanafunzi apande mche mmoja nyumbani ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo linalotoa malighafi za viwandani na kuongeza ajira katika halmashauri hiyo.

Msimamizi wa Shamba, Egata Makanja, amesema zao hilo linaweza kustawi katika mazingira yenye mvua kati ya milimita 2,000 na 2,500 na nyuzi joto 20 hadi 35 au wastani wa 27 na unyevunyevu wa asilimia 80 na mwanga wa jua wa saa 2,000 kwa mwaka.

Aidha, Makanja alisema zao hilo linaweza kupandwa na mazao mengine ya chakula mwanzoni na kuanza kuvunwa likiwa na miaka mitano kwa kipindi cha miaka 30.



Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akiwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Hashil Abdallah (kushoto), wakiangalia mpira uliochakatwa baada ya kugemwa walipotembelea shamba la mpira la Kalunga, Mang'ula wilayani Kilombero, Morogoro mwishoni mwa wiki iliyopita kuangalia jitihada za kuliendeleza zao hilo zinazofanywa na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC). **PICHA: WUVB**

# Bodi yatenga bil. 100/- kununua mazao

**Na Christina Mwakangale**

BODI ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), imesema imetenga Sh. bilioni 100 kununua mazao ya wakulima kwa lengo la kupunguza mfumuko wa bei za vyakula.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Salum Awadh, aliyasema hayo hivi karibuni wakati akizungumza kwenye kikao na wadau wa kilimo, kilichofanyika Dar es Salaam.

Alisema wamejipanga kununua angalau viwanda kutoka asilimia 30 hadi 75 kwa mazao yaliyopewa kipaumbele ambayo ni ngano, alizeti, soya, mahindi na mchele.

"Tumejipanga kutekeleza ujenzi wa maghala kila wilaya nchini na kununua mazao kisha kupeleka sokoni unga wa sembe, dona, mafuta ya alizeti, siagi ya korosho, mtama, maharage na asali," alisema Salum.

Alifafanua kwamba mikakati mingine iliyo nayo bodi hiyo ni kuanza ujenzi wa kiwanda cha mhogo Mkata mkoani Tanga, kitakachokamilika Juni, mwaka huu.

Meya wa Ubungo, Bakari Nyaigesha, alisema kinachowaangusha wakulima ni kila mmoja kujifungia peke yake badala ya kupeleka mazao CPB ambayo ina mameneja kila mkoa.

"Tutoke sasa tukatafute fursa, kwani hata zao la muhogo linakwenda kupaa zaidi kiuchumi kwa sababu ya kiwanda cha zao hilo kilichopo Mkata," alisema Nyaigesha na kuongeza kuwa Bodi ya CPB imekuwa msaada hata kwa wale wanaopeleka mazao yao nje ya nchi.

# Wauguzi wafukuzwa kazi madai ya uzembe

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAUGUZI wawili wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Masasi ya Mkomaindo, Pascal Mnyaru na Joyce Nkane, wamefukuzwa kazi baada ya kukutwa na kosa la kusababisha kifo cha mjamzito kwa kushindwa kupatiwa huduma kwa wakati.

Uamuzi huo ulitolewa na Baraza la Madiwani wa Mji wa Masasi ambao kwa kauli moja waliridhia na kusema wauguzi hao wamefanya uzembe.

Akitangaza mwishoni mwa wiki katika kikao cha baraza la madiwani baada ya wajumbe wa kikao kugeuka kuwa kamati kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali ya watumishi, Makamu Meya wa Halmashauri hiyo, Mbaraka Kodo, alisema baraza limeketi pamoja na menejimenti na kukubaliana kuwa watumishi hao wafukuzwe kazi.

Kodo alisema shauri la watumishi hao lilifika katika kamati ya menejimenti ya halmashauri na baadaye kupelekwa katika Baraza la Madiwani ili kuomba ridhaa ya kujadiliwa na uamuzi uliotolewa na baraza ni kufukuzwa kazi.

Alisema wauguzi hao, ambao wote ni wauguzi waandamizi katika Hospitali ya Mkomaindo, wanadaiwa kusababisha kifo cha mjamzito kwa kushindwa kumpa huduma za afya kwa wakati, hivyo wanafukuzwa kazi.

"Baraza la Madiwani linaridhia kwa pamoja kuwa wauguzi hawa wafukuzwe kazi kwa sababu wamefanya uzembe katika utumishi wao na kusababisha mjamzito kabla ya kujifungua kupoteza maisha kwa kushindwa kupatiwa huduma kwa wakati," alisema Kodo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji Masasi, Dk. Salumu Gembe, alisema eleza kuwa maamuzi yaliyofanywa na kikao hicho ameyapokea kwa mikono uamuzi umefanywa kwa sababu shauri la watumishi hao lilishapita kwenye vyombo vyote husika vya kiutumishi na kilichokabaki ni uamuzi wa mwisho wa Baraza la Madiwani kama mwajiri.

Alisema kabla ya uamuzi huo, mapema mwaka jana baada ya tukio kutokea katika hospitali hiyo mjamzito huyo kupoteza maisha, timu ya bodi ya wauguzi nchini ilifika na kufanya uchunguzi na kubaini watumishi hao walifanya uzembe uliosababisha mjamzito huyo kupoteza maisha.

Dk. Gembe alisema inasikitisha kupoteza watumishi katika idara ya afya lakini kwa sababu tayari uamuzi umeshafanyika na ni wazi kuwa wauguzi hao wamebainika kufanya uzembe huo, hivyo walipaswa kufukuzwa kazi kama uamuzi ulivyofanyika.

Diwani wa Mkomaindo, Ally Salvatory, alisema mara kadhaa wamepokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi juu ya wauguzi wa hospitali hiyo kutoa huduma kizembe kwa wagonjwa hivyo uamuzi uliofanywa wa kuwafukuza kazi ni sahihi.

## Wapewa somo la kuchangamkia fursa ya mafunzo

**Na Oscar Assenga,** TANGA

VIJANA wa Jiji la Tanga, wamepewa somo la kuchangamkia fursa ya mafunzo mbalimbali ya ubunifu na ujasiriamali yanayotolewa katika maeneo yao ili kuwasaidia kukua.

Mwazilishi wa Taasisi ya Tanzania Open Innovation Organization (TOIO), Shaukatali Hussein, akizungumza jana kuhusu mradi katika mafunzo ya ubunifu na ujasiriamali ambayo yanaendelea kwenye Shule ya Sekondari Tanga.

Mafunzo hayo yanaendeshwa na TOIO, chini ya ufadhili wa Shirika la Foundation Botnar.

Alisema kwamba ubunifu ndiyo silaha pekee ambayo inaweza kuwainua vijana kiuchumi uwapo wataizingatia kwa umakini na kujituma hasa kutokana na utandawazi hivyo wanapaswa kuchangamkia fursa mbalimbali zinazotolewa.

"Dunia ya sasa ubunifu umekuwa muhimu kwa jambo lolote ambalo linafanywa hivyo niwahimize vijana kuona umuhimu wa kuchangamkia fursa zilizoko kwenye maeneo yenu hususani miradi inayoanzishwa," alisema.

Aidha, alisema taasisi hiyo imejikita kuhakikisha inafanya kazi ya kuhamasisha vijana kuchangamkia fursa mbalimbali ikiwamo kwenye sekta ya kilimo, afya, elimu, pikipiki za umeme, taa za sola na ubunifu kwa kuwapatia vijana mafunzo.

"Katika mradi huu tumepanga kuwafikia vijana 900 kwa kata zote 27 za Jiji la Tanga na mpaka sasa vijana tumewafikia vijana 170. Tunaamini tutawafikia wote hivyo nitoe wito kwa wazazi na walezi kuwahimiza vijana wao kuchangamkia fursa hii," alisema.

Hata hivyo, alisema mafunzo wanayopatiwa vijana hao ni katika fursa za kilimo, afya na teknolojia mbalimbali jinsi ya kuunda na kutengeneza vitu mbalimbali na pia mafunzo hayo yanapatikana bila gharama yoyote.

Awali akizungumza mmoja wa wanafunzi wanapata mafunzo hayo, Cedrick Samwel, mwanafunzi wa kidato cha nne, alisema mambo wanayofundishwa ya ubunifu yatakuwa chachu kubwa kwao kuwa wabunifu wakubwa ndani na nje ya nchini hapo baadaye.

Vilevile alisema wamekuwa na mradi wa kutumia mtandao kuwasaidia wagonjwa kuwasiliana na madaktari hospitalini hatua ambayo inapunguza muda wa mgonjwa kufika na kumkosa na kurudi hivyo kumwondolea usumbufu.

Pia alisema kwamba mradi huo umekuwa chachu kwao kwani wamekuwa wakijifunza pia namna ya kutengeneza baiskeli na pikipiki za kutumia umeme ambazo zitaweza kuja kuisaidia jamii siku zijazo.

# Bil.19/- zatengwa ujenzi wa jengo la jemolojia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amesema serikali imetenga Sh. bilioni 19 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa nane la kituo cha jemolojia kilichoko Mkoa wa Arusha.

Aidha, ametangaza kiama kwa baadhi ya wafanyabiashara wa madini katika Mkoa wa Kigoma wanaojihusisha na biashara haramu ya kutorosha madini katika masoko ya Segese, Nyamsege pamoja na Kakora. Aliyasema hayo jana jijini Arusha, wakati wa mahafali ya kwanza ya stashahada katika Kituo cha Jemolojia Tanzania kilicho chini ya Wizara ya Madini ambapo wahitimu 39 wamehitimu katika fani mbalimbali za uongezaji thamani madini ya vito.

"Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa shilingi bilioni 19 ambazo zitakuja kwa awamu tatu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa nane ambalo litakuwa na mabweni, karakana, ukumbi wa mikutano na kituo kidogo cha wafanyabiashara wa madini kwa ajili ya wanafunzi kujifunza zaidi.

"Lengo la kujenga jengo hilo ni kwa ajili ya kupanua wigo wa kudahili wanafunzi wenye zaidi katika sekta madini kwa maslahi mapana ya taifa. Lakini wahitimu watakaohitimu wakalete mabadiliko katika sekta ya madini hapa nchini," alisema.

Alisema wamefanikiwa kuchangia pato la taifa asilimia 7.3 hadi kufikia mwaka 2022 na kwamba lengo ni kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2025.

Kwa mujibu wa Biteko, wizara hiyo imetoa Sh. milioni 716 kwa ajili ya mafunzo ya kuwaongezea ujuzi wakufunzi katika chuo hicho ambapo Sh. milioni 398 zimeshatumika katika kuwanoa wakufunzi hao.

Kuhusu wafanyabiashara wanaofanya biashara haramu ya kutorosha madini mkoani Kigoma, Biteko alisema wameshaunda timu maalum na ipo mkoani Kigoma kwa ajili ya uchunguzi na watakaobainika kuhusika na utoroshaji huo watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Aidha, kwa upande wa wahitimu hao Biteko alisema serikali itawapa ushirikiano na kuwataka kwenda kuwa chachu ya mabadiliko katika sekta ya madini hapa nchini.

"Nendeni mkafanye kazi na sisi serikali tuhakikisha tunaweka mazingira mazuri ya uzalishaji wa maligahafi kwa ajili ya viwanda vyetu vya ndani ili ufanisi wa kazi zenu ziweze kuwa na tija," alisema.

Kaimu Mratibu wa Chuo hicho, Daniel Kidesheni, alisema awali walisajili wanafunzi 78 wa stashahada lakini kutokana na matatizo mbalimbali ni wanafunzi 39 pekee wameweza kuhitimu.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Anna Shinini, akizungumza na wanachama wa jumuiya hiyo kwenye kata ya Endonyongijape juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Ridhiwani aagiza kuanza upimaji ekari 2,260 za kijiji

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amemwagiza Kamishna Msaidizi wa Ardhi, Mkoa wa Manyara, kuanza mchakato wa kupima ekari 2,260 za ardhi ya Kijiji cha Kirudiki kilichoko Wilaya ya Babati ili kuruhusu maeneo hayo kugawanywa kwa wananchi.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wananchi wa kijiji hicho juu ya mgogoro kati yao na mwekezaji wa Shamba la Amir Estate.

"Kamishna Msaidizi wa Ardhi, yatambueni maeneo haya na kuyapima. Fanyeni upimaji haraka ili tuwape wananchi. Katika hili, atakayekiuka sheria na kuvamia kwa mwekezaji atachukuliwa hatua za kisheria," alisema.

Shamba la Amir Estate lilifutwa Novemba 4, mwaka 2015 na Rais (Hayati Dk. John Magufuli).


Kuhusu hoja ya fidia ya Sh. milioni 790 anayotakiwa kulipwa mwekezaji ili aondoke, Naibu Waziri huyo aliwaahidi wananchi hao ameichukua hoja yao na ataiwasilisha kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Awali akizungumzia mgogoro huo, Diwani wa Kiru, Benjamin Kremu, alisema tathmini iliyofanywa ili walipwe fidia, ilithaminisha miti 235, ambapo kila mti ulitakiwa kulipwa fidia ya Sh. 300,000 na kila daraja lilithaminishwa na kutakiwa kulipwa Sh. milioni 60.

Alisema tathmini ya pili ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, inaonyesha fidia hiyo ilipaswa kuwa Sh. bilioni 1.2, badala ya Sh. milioni 790 ya awali inayotajwa.

Diwani huyo alimwomba Naibu Waziri huyo kuwasaidia kumaliza mgogoro huo kwa kuwa polisi wakiingia kijijini hapo kulinda usalama, hutumia nguvu kwa kupiga mabomu ya mkono, ambapo waathirika wakuu huwa ni watoto na wanawake.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, alisema masuala yote ya kiusalama yaliyogusiwa ameyachukua atayafanyia kazi.





# Wataka mikakati kumwinua mtoto wa kike kimasomo

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WADAU wa elimu wameishauri serikali kuweka mikakati madhubuti katika kuhakikisha wanamwinua mtoto wa kike ili aweze kufaulu masomo ya sayansi.

Wito huo umetolewa na Meneja Mradi wa Chomoza Stem, Mwanaidi Omari, wakati wa wiki ya kimataifa ya sayansi na mtoto wa kike.

Chomoza stem ipo chini ya shirika lisilo la kiserikali la Adilisha.

Mwanaidi alisema serikali kwa kushirikiana na wadau inatakiwa kuimarisha miundombinu shuleni sambamba na usawa wa kijinsia katika masomo ya sayansi.

Alisema kutokana na utafiti uliofanywa na Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa mwaka 2022 unaonyesha kwamba wanawake pamoja na watoto wa kike wanaoshiriki katika utafiti wa kisayansi ni asilimia 30 pekee hali inayoonyesha ushiriki wao kuwa hafifu.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau inatakiwa kuimarisha miundombinu shuleni sambamba na usawa wa kijinsi katika masomo ya sayansi.

Aidha, alisema kupitia mradi wa Chomoza Stem wamefungua maabara maalumu kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wa kike kujifunza masomo mbalimbali yakiwamo ya Biolojia, Fizikia, Kemia pamoja na Hesabu kwa vitendo ikiwa ni hatua ya kuwasaidia kufikia malengo yao pamoja na kuinua jinsia hiyo katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia.


Vilevile alieleza kuwa katika hatua za awali wanatarajia kufungua maabara hizo pia katika wilaya za Nyamagana pamoja na Ilemela ambapo watawafikia wanafunzi hao na kufanya majaribio yao bila malipo yoyote.

Baadhi ya walimu na wakufunzi wa masomo ya sayansi mkoani Mwanza waliomba serikali kuhakikisha wanarekebisha sera ya ufaulu wa mtoto wa kike ili kumwezesha mtoto huyo kufikia malengo ya kuwa mwanasayansi.

"Katika kipindi hiki tumekuwa tukishuhudia mwanafunzi wa kike anafaulu kwa alama za daraja la pili lakini anapangwa kusoma masomo ya sanaa ilihali angepangiwa kusoma masomo ya sayansi ili kutimiza ndoto zake," alisema Ever Eliakulwa mwalimu wa sayansi.

Elizabeth Makalanga ni Mwalimu Mkuu Shule ya Sekondari Makalanga alisema wadau wa elimu wanatakiwa kushirikiana na serikali kuboresha miundombinu ya kujifunzia masomo hayo sambamba na vifaa katika baabara.

Naye Daktari Heaven Chitemo ambaye ni Mkufuzi wa Chuo Kikuu Kishirikishi cha Afya na Sayansi Bugando alisema vilevile jamii inatakiwa kuelimishwa juu ya usawa wa kijinsi katika elimu.




Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Ziwa, Joseph Mutalemwa, akikabidhi gari mjini Kahama kwa Samson Daniel aliyejishindia Ndinga la Kishua kutoka Tigo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ukosefu wa vitambulisho NIDA wakosesha vikundi mikopo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UKOSEFU wa namba ya vitambulisho vya taifa kwa wanachama wa vikundi vya ujasiriamali katika Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imesababisha vikundi hivyo kuendelea kukosa mikopo na kushindwa kukua kimtaji.

Hali hiyo imesababisha wajasiriamali hao kuingia kwenye mikopo umiza yenye riba kubwa Diwani wa Ikinda, Matrida Musoma aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri hiyo cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Alisema kama Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) haitashughulikia tatizo hilo kutaendelea kuwapo kwa malalamiko ya vikundi kukosa mikopo.

Alisema wamewehamasisha vijana, kinamama na watu wenye ulemavu kujiunga katika vikundi vya ujasiriamali ili waweze kukopeshaka na halmashauri fedha za kukuza biashara zao, lakini wanakosa sifa ya kupata mikopo hiyo baada ya kukosekana kwa namba zao.

Alisema hata wazazi wenye watoto chini ya miaka mitano wameshindwa kupata vyeti vya kuzaliwa vya watoto wao kwa sababu wanatakiwa kujaza namba ya kitambulisho vya taifa katika fomu ya kuomba cheti na hii itasababisha wale wenye umri wa kwenda shule kuchelewa kuanza masomo.

Akijibu hoja hizo, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Judica Sumari alisema, mfumo wa utoaji wa mikopo katika vikundi vya wajasiriamali umeunganishwa na mfumo wa NIDA hivyo bila kuwa na kitambulisho au namba kwa mwanakikundi hawawezi kupata mikopo.

Alisema mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya vikundi 11 vya vijana na kinamama vilipata mkopo huo sawa na Sh.milioni 120 kati ya hivyo vikundi nane vya vijana vilipata Sh. milioni 96 na vikundi vitatu vya kinamama vilipata Sh. milioni 23.5 na mwaka huu wa fedha wametenga Sh.milioni 453.

Alisema vikundi vya kinamama vinaongoza kufanya marejesho kulinganisha na vikundi vingine na wamekuwa wakishirikiana na madiwani wa kata kuwahamasisha kurejesha mikopo.

# Samia awataka waandishi kuuliza maswali kupata ufafanuzi

**Na Richard Makore,** MWANZA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka waandishi wa habari mkoani Mwanza kuuliza maswali mbalimbali ili kupata ufafanuzi kutoka serikalini kuhusiana na masuala yanayohusu nchi.

Alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari moja kwa moja kwa njia ya simu kupitia kwa Msemaji wa Serikali, Greyson Msigwa, alipozungumza na waandishi wa habari mkoani Mwanza.

Rais Samia aliwataka waandishi wa habari kumuuliza Msigwa maswali mbalimbali waliyonayo na kupata majibu sahihi na kwamba atakayoshindwa kuyatolea majibu atakwenda mwenyewe mkoani Mwanza kuyajibu ama atatuma Waziri Mkuu kwenda kuyajibu.

Alisema Tanzania itajengwa na watu wote wakiwamo waandishi wa habari, wakulima, wananchi pamoja na Rais mwenyewe.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Msigwa alitolea ufafanuzi wa masuala mbalimbali ndani ya serikali ikiwamo sekta ya afya, elimu, miundombinu, sekta ya kilimo pamoja na uvuvi.

Alisema serikali itaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ikiwamo ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), Daraja la Magufuli lililoko mkoani Mwanza pamoja na ujenzi wa Meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu.

Katika hatua nyingine, Msigwa alishuhudia Meli ya Mv Mwanza Hapa Kazi Tu, ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 82, ikishushwa ndani ya maji.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, akizungumza katika hafla ya kuingiza meli majini, aliitaka Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), kuhakikisha inajipanga kuendelea kuboresha bandari na gati mkoani Mara katika Ziwa Victoria ili meli hiyo iweze kufanya kazi itakapoanza safari zake.

Mwakibete alisema serikali imewekeza kwenye miradi mikubwa ya maendeleo inayotekelezwa na MSCL kwa lengo la kuboresha huduma ya usafiri wa abiria na mizigo kwa njia ya meli.

Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL, Erick Hamisi, alisema kukamilika kwa meli hiyo itahudumia bandari zote kuu katika Ziwa Victoria zikiwamo za Kemondo, Bukoba, Mwanza, Musoma na Portbell na Jinja za nchini Uganda pamoja na Kisumu nchini Kenya.

Hamissi alisema meli hiyo ina uwezo wa kubeba abiria 1,200, tani 400 za mizigo na magari madogo 20 hadi kukamilika kwake na itagharimu kiasi cha Sh. bilioni 109.

Nipashe
# TESA
Jumanne Februari 14, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

## Tanga kumekucha ni mradi shule bora kuanza kwa kasi



## Wilayani Kibiti ni mwaka wa elimu yatangazia vita utoro, mimba na njaa

Ukurasa 13

SAYANSI

**NA CHRISTINA MWAKANGALE**

MAAJABU VIJANA WABUNIFU

# Waibua vifaa kuboresha oksijeni kunusuru wanaopumulia mashine

## •Vipo vya kusimamia moyo wa watoto njiti

UBUNIFU wa vitu kuanzia bidhaa na huduma mbalimbali ni miongoni mwa vipaji ambavyo kila binadamu huzaliwa navyo.

Ingawa kazi za ubunifu na ugunduzi zinafanyika, changamoto ni namna ya kuziendeleza, kuzibadili kuwa fursa na kuleta suluhisho kwenye matatizo ya jamii na taifa lenye hazina ya wataalamu hao.

Godfrey Sospeter (22) na Neema James (21), wanafunzi wa Taasisi ya Teknolojia Dar-Es-Salaam (DIT), kwa nyakati tofauti wanaonyesha namna elimu waliyoipata inavyoendeleza ubunifu na ugunduzi wao kuelekea kupata suluhisho kwenye matatizo ya jamii hasa sekta ya afya.

Kwenye mahojiano na Nipashe hivi karibuni, wanaeleza namna walivyobuni njia ya kuboresha afya kwa kuunda kifaa cha kupima ubora wa oksijeni iliyomo kwenye mitungi inayotumiwa na wagonjwa wenye changamoto za kupumua.





Godfrey Sospeter na Neema James: **PICHA CHRISTINA MWAKANGALE**

**KIPIMA OKSIJENI**

Godfrey mwanafunzi wa mwaka wa tatu anayesoma shahada ya uhandisi umeme akijiunga na chuo baada ya kumaliza kidato cha sita, alikosoma Fizikia, Kemia na Hisabati.

"Niliyamudu masomo ya sayansi ambayo yanasemekana kuwa magumu. Ninaamini kuwa hakuna kigumu kilichovumbuliwa, kuundwa na mwanadamu nikiwamo mimi."

"Hivyo fikra ndizo zimenipa mwongozo mpaka hatua niliyopo. Natarajia kuwa kiongozi bora katika kutetea utumiaji wa nishati safi kwa mazingira kwa Tanzania na Afrika," anasema Godfrey.

"Tulianza na tafiti katika hospitali mbili za wilaya, Kigamboni na Amana, Agosti 2022. Tangu kufanya tafiti mpaka kutengeneza vifaa tumetumia takribani siku 30. Tumefanya kazi zote hizi ndani ya DIT kwenye 'design studio. Lakini hatujafanikiwa kuvifikisha kwenye hospitali hadi sasa."

Anasema kifaa walichobuni kinaitwa kifuatilia ubora wa oksijeni. Na kwamba kina king'ora kinachotoa sauti endapo kiwango cha oksijeni si kile kinachotakiwa kuwekewa kwa mgonjwa, kulingana na viwango vya Shirika la Afya Duniani (WHO).

Anaeleza kuwa lazima kiwe cha asilimia 91 hadi 99 na si chini ya hapo, anaeleza mbunifu, anayeongeza kuwa walitafiti

na kugundua kuwa kuna vifaa vingi vya kuzalishaji oksijeni lakini havifanyiwi ukarabati au vina hitilafu na kuzalisha hewa iliyo chini ya kiwango cha WHO

Anaeleza kuwa baada ya kutengeneza kifaa hicho, wanaendelea kukifanyia maboresho na kwamba wamebaini kuwa kifaa hicho, hakipo kwenye hospitali nyingi nchini zikiwamo yalikofanyika majaribio licha ya kwamba katika nchi zilizoendelea ni muhimu na hutumiwa kwenye hospitali kuupima ubora wa oksjeni kabla ya kumwekea mgonjwa.

"Tunaona kuwa kinahitajika kifaa cha bei nafuu chenye ubora wa hali ya juu kupima ubora wa kiwango cha oksijeni kwa ajili ya wagonjwa wenye mahitaji hayo," anaongeza.

Anasema uwepo wake ndani DIT, umemfanya ajifunze mengi na kufanya ubunifu wa kifaa cha kupimia ubora wa oksijeni inayotumiwa na wagonjwa wodini.

Aidha, kifaa hicho kinaweza pia kupima kiwango na ubora wa oksijeni kwenye mtungi, kabla ya kuwekea mgonjwa wodini, lakini hata eneo alipolazwa pia kufahamu ubora wa hewa anayovuta.

Godfrey anasema kitalaamu okisjeni inayotumiwa huzalishwa kwa njia tofauti na kutaja teknolojia ya kuchuja hewa iliyoko kwenye mazingira watu wanayoishi kupata kiwango kinachohitajika.

Anasema hewa ina gesi za nitrojeni, oksijeni, kaboni na hydorojeni na hivyo huchujwa kupata kiwango cha okisjeni anayotumia mgonjwa.

Akizungumzia malighafi zinazotumika kukiunda anasema vinapatikana nchini ambavyo ni plastiki, lakini vifaa kama 'sensors,' ving'ora vinavyotoa mlio, 'displays' na 'control unit' ambayo hufanya maamuzi na kutoa ripoti ya ubora vyote huagizwa nje.

**WANAPOKWAMA**

"Changamoto kubwa iliyopo kwa wabunifu ni kuwezeshwa ili kuendeleza kazi iliyogunduliwa ikamilike na kukidhi viwango," anasema Godfrey.

INAENDELEA UK. 12

ELIMU

NA HAMIDA KAMCHALLA, TANGA

# Tanga kumekucha ni mradi shule bora kuanza kwa kasi

TANZANIA na Uingereza zinashirikiana kufanya maboresho yatakayowezesha kila mtoto kupata msingi bora wa elimu ya awali, ili kutoa fursa ya kufikia ngazi ya shule ya msingi hadi sekondari.

Katika hatua zote kila mtoto, anasoma kupitia utaratibu wa elimu shirikishi inayogusa watoto wenye mahitaji maalumu na wale wenye viungo na utimilifu wa maumbile ili kuhakikisha wote, wanakwenda pamoja kwa mafanikio.

Mratibu wa Mradi wa Shule Bora Mkoa wa Tanga, Thomas Aikaruwa, anabainisha hayo anapozungumza na Nipashe na kusema kuwa mradi huo unalenga kufanikisha kuwa elimu jumuishi inaboreka na kutolewa kwa watoto wote.

Anasema Mradi wa Shule Bora unafanikishwa kwa pamoja baina ya Uingereza kupitia UK AID na Tanzania ukilenga kuunga mkono miradi ya elimu, ukitekelezwa katika mikoa tisa.



Wanafunzi na mwalimu wakifurahia mazingira bora ya usomaji na ujifunzaji.

Aikaruwa anasema unapokea utaalamu wa kiufundi kutoka Cambridge Education ikishirikiana na mashirika ya ADD International, International Rescue Committee pamoja na Plan International.

Anasema shule bora pia unalenga kuiunga mkono serikali katika kuinua kiwango cha elimu jumuishi pamoja na kuweka mazingira salama ya kujifunzia kwa wanafunzi wote wa kike na wa kiume kuanzia shule ya awali, msingi na mwanzoni mwa sekondari.

Kwa kushirikiana wadau hao mradi huu utafanya maboresho yatakayowezesha kila mtoto kupata msingi mzuri katika elimu yake ya awali, ili kuzitumia fursa kwa kutoa mchango wake katika ukuaji wa nchi na maendeleo yake.

Aidha, Aikaruwa anataja mikoa tisa ambayo ni Dodoma, Katavi, Kigoma, Mara, Pwani, Rukwa, Simiyu, Singida na Tanga kuwa ndiyo wanufaika wa mradi huo.

"Mradi unalenga katika maeneo manne ambayo ni kujifunza kwa watoto wote shuleni, kufundisha ambapo mfuko wa msaada wa UK utaunga mkono na kuimarisha kazi ya ufundishaji."

"Jumuishi pamoja na kujenga mfumo ambao mfuko wa UK AID utaunga mkono serikali na kuimarisha ili kupata au kuwa na thamani ya fedha katika utoaji wa elimu katika ngazi zote kuanzia chini hadi taifani," anasema

Mratibu wa Mradi wa Shule Bora Mkoa wa Tanga.

Hata hivyo, anasema jumuishi ni kipaumbele cha mradi huo ambao utawatupia macho kwa karibu wanafunzi wenye mahitaji maalumu na wale wanaotoka katika mazingira magumu na kuwawezesha kuwa shuleni katika mazingira bora na salama hadi kufikia elimu ya sekondari.

"Hii ni pamoja na kuwashirikisha wazazi, walezi na jumii katika kuboresha usalama wa shule na kuondoa migogoro, kuhakikisha walimu wanazungumzia mambo ya jinsia na upatikanaji wa mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu."

"Pia kutayarisha mazingira salama na kuwaunga mkono wasichana kushiriki pamoja na kujadili mambo yanayowahusu, lakini



Kusoma kwenye darasa bila viti na miundombinu muhimu hukwaza wenye mahitaji maalumu . **PICHA ZOTE: HAMIDA KAMCHALLA**

kuwasaidia katika kipindi cha hedhi," anabainisha Aikaruwa.

Aikaruwa anabainisha kwamba shule bora itafanya kazi moja kwa moja na mamlaka za serikali za mikoa na halmashauri pamoja na shule katika mikoa husika yenye changamoto nyingi kama ilivyopendekezwa na kukubalika na serikali katika kuboresha elimu.

Anasema, inakadiriwa kuwa mradi huu utawafikia watoto takribani 4,000,000 kati yao nusu ni wasichana, mabadiliko na ubunifu yataonekana na kutathminiwa katika ngazi za chini ambazo walengwa muhimu watapatikana katika shule zote za msingi zitakazofikiwa.

Aidha, anasema, wakati watoto wengi wakijiunga na kuendelea na masomo, matokeo ya elimu nchini yamekuwa na changamoto nyingi na kwamba ni asilimia nane ya wanafunzi elimu ya msingi ndiyo wanafikia kiwango cha taifa cha kujua kusoma na kuandika, huku asilimia 12 wanafikia kiwango cha taifa cha kuwa na ujuzi wa kujumlisha na kutoa.

"Kwa kiasi fulani, hii inachangiwa na ongezeko la uhitaji wa elimu msingi sambamba na ongezeko la idadi ya watu, kunakosababisha ongezeko la uwiano wa walimu na wanafunzi ambako kwa sasa ni wastani wa wanafunzi 62 kwa kila mwalimu mmoja katika shule za msingi za serikali," anafafanua.

Wizara ya Elimu inaeleza kuwa mradi wa shule bora unalenga matokeo katika ngazi ya kitaifa ambapo utawezaesha kupata msaada wa kiufundi kwa serikali pamoja na utekelezaji wa mradi wa Lipwa kwa Matokeo (EPforR II).

Inafafanua kwamba malengo ya utekelezaji wa kitaifa yanapangwa kwa pamoja kati ya serikali na wafadhili huku utoaji wa fedha ukihusisha malengo yaliyofikiwa.

Kwa ujumla inasisimua mabadiliko ya kimfumo kama yale ya mawazo sawa wa walimu na kugawa vitabu, lakini pia shule bora pia itafadhili matokeo muhimu yatakayotokana na vigezo vilivyothibitishwa kutoka katika mradi wa EPforR ambavyo vitatumika katika kutoa fedha na wafadhili wengine.

Kwa ufadhili wa serikali ya Uingereza, kupitia mfumo wa UK AID, gharama za mradi zitakuwa na bajeti ya Paundi milioni 89, takribani bilioni 271 na utafanya kazi hadi ifikapo mwaka 2027, kwa mujibu wa Wizara ya Elimu.

Ili kufanikisha na kueneza ufahamu wa mradi huo, mafunzo ya shule bora yanatolewa kwa wanahabari takribani 30 na maofisa habari wa halmashauri za wilaya tisa pamoja na maofisa habari mkoa yanafanyika Korogwe na kusimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

# Waibua vifaa kuboresha oksijeni kunusuru wanaopumulia mashine

INATOKA UK. 11

**KIPIMO CHA NJITI**

Neema, kama Godfrey amesoma sayansi Fizikia, Jiografia na Hisabati- PGM akisoma shahada ya Electronics na Mawasiliano ya Angani, mwaka wa tatu chuoni DIT.

Anasema amesoma sayansi akitamani kuwa na mchango katika jamii akibuni vifaa kupunguza matatizo kwenye sekta mbalimbali.

Neema na wenzake Gilbert Msumba, Nasekile Fungo na Kheri Kajuna, walitembelea hospitali za Kigamboni na Amana , ziara iliyowawezesha kungundua kifaa cha kufuatilia mapigo ya moyo na joto la mtoto njiti.

"Ni baada ya kutembelea wodi ya uangalizi maalumu ya watoto njiti au ICU ya njiti wenye umri wa siku 0 hadi 28," anasema Neema.

"Tuligundua kuwa ufuatiliaji au monitoring kwa watoto njiti unafanyika kwa ugumu sana hasa kwa hospitali zilizoko kijijni. Hivyo, ubunifu wetu unaoitwa 'portable neonatal monitor' ni kifaa kitatumika kufuatilia mapigo hayo ya moyo na joto la mtoto njiti. Ni chepesi, bei nafuu ya Sh. 140,000 na kina mifumo ya ving'ora inayomjulisha muuguzi kumhudumia mtoto na pia kinaweza kuchajiwa na kutumiwa eneo lisilo na umeme," anasema Neema.

**WANAPOSHINDWA**

"Changamoto kubwa wabunifu tunayopata kukosa 'jukwaa la kutuandaa au kutupa mwongozo sahihi wa kufanikisha ubunifu wetu. Lakini, pia wabunifu wengi kukata tamaa mapema wanaposhindwa kuendeleza kazi zao wakikosa uwekezaji," anasema msomi huyo.

"Ninaamini hiki kifaa kitaboresha afya ya mtoto njiti kwa hatua kubwa kwani kinaweza tumika katika vijiji na pia na Mtanzania yeyote anayehumia motto huyo hata kama hana ujuzi wa hali juu," anaongeza Neema.

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBITI

# Wilayani Kibiti ni mwaka wa elimu yatangazia vita utoro, mimba na njaa

Ni malengo ya taifa, kila mzazi na mlezi anapompeleka mwanawe shule, afahamu na ufaulu ili baadaye apate kujitegemea na kumudu maisha yake na kuleta maendeleo ya nchi.

Siyo matarajio ya wengi kusomesha watoto halafu wawe wazururaji mtaani na kufanya uhalifu.

Ndivyo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani, baada ya kuona kuna vitu vinashusha ufaulu inaweka maazimio ya kuvikabili.

Kibiti ni kati ya halmashauri tisa za mkoa wa Pwani, ni moja ya maeneo yanayohitaji jitihada na mikakati zaidi ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Katika kikao cha wadau wa elimu kinachofanyika hivi karibuni kwenye Sekondari ya Kibiti, suala la namna ya kukabiliana na mimba za utotoni, utoro na wanafunzi kujishughulisha na biashara wakati wa masomo linapewa nafasi.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kibiti Meja Edward Gowele, akiwa mwenyekiti, anaeleza kuwa msingi wa maendeleo popote ni elimu na kwamba kiwango hafifu cha ufaulu kwenye mitihani ya kitaifa kinachangia maendeleo madogo ya kitaaluma.

Anasema Kibiti inahitaji mabadiliko kuanzia kwa wazazi na walezi ili kuwafuatilia kwa karibu watoto wao na kudhibiti utoro unaosababisha wasifanye vizuri darasani.

Anawataka wazazi na walezi kujenga ushirikiano kuwachukulia hatua watoto wanaokutwa kwenye maeneo ya biashara muda wa masomo.

"Tushirikiane kuwafuatilia tunapoona watoto au mtoto anafanya biashara kipindi cha masomo, hata kama siyo mwanao we chukua hatua na mzazi wake akikujia juu tupate hizo taarifa, bila kufanya hivi elimu Kibiti itaendelea kushuka," anaonya Kaimu Mkuu wa Wilaya.

Aidha, anaeleza kuwa ili kudhibiti ongezeko la mimba shuleni ni vema wazazi kutoa ushirikiano kwa wale wanaowaoa na kuwapa mimba wanafunzi.

Kaimu Mkuu wa Wilaya anawageukia pia viongozi wa dini kuzungumzia suala la elimu wakiwa kwenye nyumba za ibada ambapo kwa kufanya hivyo wataleta tija kwa kuhamasisha waamini watoto hadi wazee.

Anasisitiza suala la wazazi na walezi kuona umuhimu wa kuchangia chakula shuleni ili wanafunzi wasome kwa bidii wakiwa wameshiba badala ya ilivyo sasa kwa shule nyingi ambazo hazijawa na utaratibu huo.



Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kibiti Meja Edward Gowele, akiwa katika mikutano ya kuandaa mikakati ya kuboresha elimu. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

"Tuweke kiasi cha fedha kwa ajili ya watoto wetu, kuwanunulia mahitaji ya shule lakini kuchanga fedha za chakula wasisome huku wakiwa na njaa," anasisitiza.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, anaeleza kuwa kikao cha wadau wa elimu kimekuwa kikifanyika kila mwaka lakini bado kuna mambo yanawarudisha nyuma.

Mavura anasema katika kikao cha mwaka huu wamejikita zaidi kwenye vikwazo vya ufaulu, kujiuliza na kujadili kwanini vinaendelea na nini kifanyike kuviondoa.

Anasema serikali inaweka fedha nyingi katika sekta ya elimu hivyo ni jukumu la jamii kuungana kumwondolea vikwazo na kupambania ufaulu wa mwanafunzi ngazi ya msingi na sekondari.

"Tujifikirie zaidi kuendeleza elimu hapa Kibiti kwa kuwashirikisha wadau, ushirikishwaji ni muhimu kwenye maendeleo ya elimu, nataka niache alama katika sekta hii, ufaulu uongezeke na kila mzazi aone umuhimu wa kusomesha mtoto wake," anasema Mavura.

Aidha, anasema wapo baadhi ya wazazi na walezi wanatakiwa kubadilika kwani wakati mwingine serikali inatumia nguvu kuwarudisha wanafunzi shule lakini baada ya muda wanaonekana mitaani kwenye sehemu za biashara muda wa masomo hali hiyo ni kuendelea kuidumaza elimu.

"Tunatumia nguvu kumrejesha mwanafunzi shuleni baada ya siku chache wanarudi kuendelea na biashara, wakikamatwa wazazi ndiyo wanaandamana kwenda kwa Mkuu wa Wilaya kuomba watoto waachiwe huru watarudi shule lakini wanarudi tena kule walikotolewa hapa hatuvuki tunatakiwa kubadilika," anasema.

Ili kukabiliana na njaa kwa wanafunzi Mavura anashauri kila shule kutumia mashamba yake kupanda mihogo na mazao mengine ya chakula.

"Watoto wanatembea umbali mrefu, wakifika shule hakuna chakula kwa hali hii hawawezi kufanya vizuri kwenye mitihani yao, tubadilike tuipe elimu kipaumbele tuungane kukabiliana na njaa kwa watoto wetu wawapo shuleni, jiiulize wewe unaweza kushinda bila kula mchana," anasema.

Katika taarifa yake Ofisa Elimu Sekondari Anna Shitindi, anasema bado kuna kikwazo cha elimu kwa wazazi na walezi kuwashawishi wanafunzi kufanya vibaya kwenye mitihani yao ya shule ya msingi kwa lengo la kukwepa majukumu ya kuwasomesha.

Kukosekana kwa chakula cha mchana nacho kinaelezwa kuwa kunashusha ufaulu, wanafunzi kupata ujauzito na upungufu wa miundombinu.

"Tamaduni zilizopitwa na wakati, kukithiri kwa utoro kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari pamoja na ushirikiano hafifu kutoka kwa wazazi na walezi katika kusimamia maendeleo ya taaluma ni kikwazo cha ufaulu," anasema.

Anasema ipo mikakati ya kukabiliana na vikwazo vya elimu ambayo ni pamoja na kuielimisha jamii umuhimu wa elimu kuwa na uelewa kuwa elimu ni haki ya msingi kwa kila mtoto hivyo waache kuwashawishi kufanya vibaya kwenye mitihani.

Anaeleza kuwa mikakati mingine ni pamoja na kuhamasisha jamii kujitoa katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali kulingana na vipaumbele.

"Katika mikakati yetu pia tumeweka suala la kuhamasisha jamii kuhusiana na umuhimu wa kuchangia chakula ili wanafunzi wapate chakula cha mchana, lakini kuhamasisha shule kulima mbogamboga kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi," anabainisha.

Aidha, anasema idara hiyo inaomba wadau wa elimu kushirikiana katika kudhibiti utoro wa wanafunzi na kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na tamaduni zilizopitwa na wakati.

Hamidu Ungando, Diwani wa Kibiti, anasema sababu zinazochangia ufaulu duni kwenye shule zilizopo katika kata yake ni pamoja na msongamano wa wanafunzi darasani.

Aidha, baadhi ya wanafunzi kutembea umbali mrefu ambao wapo kati yao wanaotembea kilometa tano kila siku na wakifika shule wanachoka na hakuna chakula wala maji.

"Kwa mwaka jana katika kata yangu wanafunzi wa kike 18 walikatisha masomo kwa mimba na watuhumiwa wengi wa mimba zao ni madereva wa bodaboda ambao wamekuwa wakiwapa lifti," anaeleza Ungando.

Ungando pia anaeleza kuwa mwamko wa elimu kwa baadhi ya wazazi na walezi ni kikwazo kwani wanapowapeleka watoto shule hawafuatilii maendeleo yao hata wanapoitwa kwenye vikao hawatokei.

"Mfano hiyo ina wanafunzi zaidi ya 2,000 kikiitishwa kikao wanaweza wakafika wazazi 200 kwa hiyo hata utekelezaji wa maazimio haufanyiki kama inavyotakiwa lakini pia hata wakitakiwa kulipa Sh. 1,000 kwa wiki ili mtoto apate hata uji kwa siku akiwa shule nayo hawatoi kama inavyotakiwa na hivyo watoto wasoma wakiwa na njaa na kuhimiza mabadiliko," anasema.

TEKNOLOJIA

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Ndivyo mawasiliano kielektroniki yanavyowaachia watu historia

## •Ni kuongeza uwajibikaji bila kuwasahau waliotumbuliwa



Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alipochukua hatua kufuatia walimu kuwaadhibu vibaya wanafunzi. **PICHA: EATV**

KUKUA kwa matumizi ya teknolojia ya kidijitali duniani kuanzia miaka ya 2000 hususan kwa nchi zinazoendelea yameleta mafanikio chanya japo si kwa sekta zote na kuchochea uwajibikaji na kuwachukulia walalamikiwa hatua.

Haya yanadhihirika baada ya taarifa za malalamiko kusambaa mitandao na kuwaibua viongozi na mamlaka zinazowasimamia na hata wakati mwingine kuongeza woga wa kufanya vitendo vya uhalifu vikiwamo kudai mlungula hasa barabarani.

Teknolojia ya kidijitali inaipa jamii uwezo wa kufikisha ujumbe na malalamiko moja kwa moja kwa viongozi wa serikali na wa kisiasa kwa kutumia mitandao ya kijamii.

Kasi ni kubwa sasa mawaziri hata viongozi wa mikoa, wilaya na taasisi za umma, kuonekana wakitoa maamuzi ya moja kwa moja, ya papo hapo mara wapatapo taarifa kuwahusu wao imekuwa ni kawaida japo pia kwa kurekodi na kuufahamisha umma.

Mfumo wa kimtandao na idadi ya watumiaji wa intaneti duniani imezidi kuongezeka huku bara la Afrika likishika nafasi ya tatu kwa wingi wa watumiaji, Ripoti ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ya hadi Desemba 2017, imeonyesha kuwa idadi ya watumiaji wa intaneti inaongezeka kufikia watu milioni 23 ambayo ni sawa na asilimia 45 ya Watanzania wote.

Inaongeza kuwa mwaka 2013 wateja walifikia milioni 9.31 sawa na asilimia 21, ikimaanisha kuwa kila mwaka kuna watumiaji wapya na uwanja hupanuka zaidi.

**KUWAIBUA VIONGOZI**

Matukio kadhaa yaliyojitokeza mapema mwaka huu, mwishoni mwa mwaka jana na hata mwaka 2021, ni dhahiri teknolojia inawafikisha wananchi karibu na viongozi wao.

Mfano, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kakanja wilayani Kyerwa mkoani Kagera anasimamishwa kazi akituhumiwa kuwachapa viboko kikatili wanafunzi wa darasa la nne.

> “Kama ambavyo tumekuwa tukiona kwenye mitandao ya kijamii imekuwa ikisambaa video hiyo ikimwonyesha mwalimu Isaya, akiwachapa watoto hao huku pembeni wakiwamo walimu wanne wakicheka na kufurahia tukio hilo,” anasema Chalamila akiwaeleza wanahabari.

Mkuu wa Mkoa Kagera, Albert Chalamila, anasema hatua hizo zinachukuliwa na uongozi baada ya video inayomwonyesha Mwalimu Mkuu Isaya Emmanuel, akiwapiga viboko watoto wawili, kusambaa mitandaoni.

“Kama ambavyo tumekuwa tukiona kwenye mitandao ya kijamii imekuwa ikisambaa video hiyo ikimwonyesha mwalimu Isaya, akiwachapa watoto hao huku pembeni wakiwamo walimu wanne wakicheka na kufurahia tukio hilo,” anasema Chalamila akiwaeleza wanahabari.

Tukio hilo, lililotokea Januari, mwaka huu siku chache kabla ya kuanza kwa masomo ya mwaka huu, mwalimu huyo anawaadhibu watoto hao kwa kosa la kutofanya kazi ya ziada ‘home work’ aliyokuwa amewapa wakati wa likizo.

Mwaka huu unashuhudia video ya watumishi wawili wa afya inayosambaa mitandaoni ikionyesha mabishano kuhusu vipimo vya malaria (MRDT), muuguzi akimlazimisha kijana wa maabara kutumia vipimo hivyo kwa mjamzito na kijana huyo akigoma akichodai kuwa vimekwisha muda wa matumizi.

Taarifa hiyo inayosambaa Januari 5, mwaka huu, inahusu watumishi hao wa zahanati huko Uyui mkoani Tabora, Rose Shirima muuguzi mkunga na James Chuchu mteknolojia wa maabara ambao wanasimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi kwa mujibu wa kanuni ya 37 ya utumishi wa umma ya mwaka 2003.

Aidha, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anaagiza mamlaka kufuatilia suala hilo na kuchukua hatua huku akidai kuwa hakuna vitendanishi vya malaria vilivyoisha muda wa matumizi.

Baada ya kauli hiyo ya Waziri Ummy, Halmashauri ya Wilaya ya Uyui ikatangaza kuwasimamisha kazi watumishi hao wawili taarifa ikitolewa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Uyui, Dk. Kija Maige.

Mwaka 2021, TAMISEMI inabainisha video inayosambaa mitandaoni ikimwonyesha daktari aliyemshona jeraha mgonjwa na kufumua mshono kwa madai ya kushindwa kulipa gharama.

Likitokea katika kituo cha afya Kerenge kilichoko Tarafa ya Magoma Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, linapata ufafanuzi wa ofisi hiyo, Septemba 4, 2021 baada ya kusambaa kwa video hiyo na kuzua mjadala mtandaoni huku Wizara ya Afya ikitoa tamko na kwamba yeyote mwenye kufahamu eneo hilo kwa kutoa taarifa na kisha kuweka namba ya simu. Taarifa zilifanikisha daktari huyo kusimamishwa kazi.

Licha ya gharama za vifurushi mwishoni mwaka jana kulalamikiwa na wananchi kudai kiwango kikubwa kwa muda mfupi, wengi wao wanajikita mitandaoni kubadilishana taarifa zikiwamo za matukio hayo ambayo yametia fora.

Tanzania imeshika nafasi ya 10 katika orodha ya nchi zenye idadi kubwa za watumiaji wa intaneti Afrika kwa mwaka 2022 kwa mujibu wa taarifa zinazotolewa na Data Reportal.

Na kwamba nchi inayoongoza ni Nigeria ambako kuna wateja milioni 109.2 wa intaneti nchini humo hadi Januari 2022.

Misri ina wateja wa intaneti milioni 75.66 ni ya pili, Afrika Kusini ya tatu ikiwa na watumiaji milioni 41.19 wa intaneti mpaka Januari 2022, ya nne, ni Morocco yenye watumiaji milioni 31.59 wa intaneti hadi mpaka Januari 2022, wakati Ethiopia iliyo na wateja milioni 29.83 wa intaneti mpaka Januari 2022 ni ya tano.



# Tanzania kunufaika na bil.120/- kutoka UN

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TANZANIA inatarajiwa kunufaika na ufadhili wa Sh. bilioni 120, kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linalojihusisha na kufadhili miradi ya mazingira (GEF) katika kutekeleza miradi ya kutunza mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kipindi cha miaka minne.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga, alibainisha hayo jana jijini hapo baada ya kufungua semina ya siku mbili ya wadau wa mazingira kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

**Shirika hilo limekuwa likitoa fedha za ufadhili wa miradi ya kuhifadhi mazingira kwa awamu saba na hivi sasa inajipanga kutoa kwa awamu ya nane.**

Alisema semina hiyo ya siku mbili inalengo la kuwakutanisha wadau wote wa mazingira Tanzania Bara na Zanzibar ili kujadiliana miradi ya kipaumbele ambayo itasaidia kutunza mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Semina hii imejumuisha wadau wote wa mazingira kutoka wizara za kisekta, sekta binafsi, taasisi za kisekta pamoja na asasi za kiraia ili kuja na miradi ambayo itapata ufadhili kutoka shirika hili la Umoja wa Mataifa katika kipindi cha miaka minne," alisema Maganga.

Kadhalika, alisema shirika hilo limekuwa likitoa fedha za ufadhili wa miradi ya kuhifadhi mazingira kwa awamu saba na hivi sasa inajipanga kutoa kwa awamu ya nane ambayo itakwenda kutekelezwa muda wa miaka minne.

"Fedha hizi kutoka GEF, zimetolewa kwa awamu saba sasa na hii ambayo inakwenda kutolewa ni ya nane, hivyo kabla ya kuanza kwa awamu ya nane tumeona kukutana kwanza na wadau ili kujadiliana kwa pamoja na kuona ni miradi gani ya kipaumbele ambayo watapendekeza kutekeleza kupitia fedha hizi ili kukabiliana na changamoto za mazingira na athari za mabadiliko tabianchi," alisema.

Aidha, alisema serikali bado inaendelea na jitihada mbalimbali za kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi ikiwamo kuhamasisha wananchi kutunza mazingira na kupanda miti.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Wadau wa Mazingira nchini, Tumain Marijani, alisema wanaipongeza serikali kwa namna ambayo imeshirikisha wadau mbalimbali kujadiliana miradi ambayo italeta tija katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa miaka minne ijayo.

Alisema: "Tunapenda kutoa wito wetu kwa mashirika mengine pamoja na wananchi kwa ujumla kuhakikisha kuwa wanaunga mkono juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi".

## 'Vijana msitumie pesa za mikopo kwenye anasa'

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIJANA wanaokopeshwa fedha zinazotokana na mapato ya ndani ya halmashauri ya asilimia 10 wametakiwa kuzitumia kwa lengo la kujikwamua kiuchumi na siyo kwenye anasa.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Ipagala mkoani Dodoma, Mohamed Keba, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na vijana wa kata hiyo waliokopeshwa mikopo inayotolewa na halmashauri.

Hivyo aliwataka kuhakikisha wanaitumia kwa malengo waliyokusudiwa na siyo kwa anasa na kuzingatia urejeshaji kwa wakati.

"Tatizo lililoko kwa vijana walio wengi wanaochukua fedha hizi wamekuwa wakizitumia kwa matumizi ya anasa huku wengine wakitoroka na fedha hizo hali ambayo imekuwa ikiwasababishia kushindwa kufikia malengo yao ya kurejesha kwa wakati," alisema.

Aidha, alisema ili kuendelea kupatiwa mikopo hiyo wanatakiwa kujitengenezea mazingira ya kuaminika itakayowafanya waweze kukopa mara kwa mara, kujiimarisha zaidi kwenye miradi wanayoifanya.

Alisema serikali ina nia nzuri na vijana ya kuhakikisha wanajishughulisha na kazi mbalimbali ikiwamo za ujasiriamali, hivyo fursa zinazotolewa za kupatiwa mikopo wanatakiwa kuzitumia kwa malengo husika.

"Tatizo lililoko kwa baadhi ya vijana wanaopewa mikopo wengi ujiingiza kwenye matumizi ya anasa na wengine kutoroka nazo hali ambayo imewaletea matatizo na baadhi yao kujificha baada ya kushindwa kurejesha mikopo hiyo," alisema.

Hata hivyo amewataka vijana hao wanaochukua mikopo kuanzisha miradi ya biashara ambayo itakayoweza kuwainua kibiashara, badala ya kuiga na kujikuta wakifilisika kwenye mitaji yao.

Aidha, aliwahakikishia pia watu wenye ulemavu kujitokeza kwa wingi kuchangamkia fursa za mikopo ya asilimia mbili inayotolewa kwa upande wao, badala ya kukata tamaa na kuwasababishia kuendelea na hali ya umaskini.

Mwenyekiti huyo pia aliomba serikali kuendelea kutoa elimu ya ujasiriamali ili wanaokopeshwa waweze kufahamu umuhimu wa mikopo hiyo na kuwafanya waweze kurejesha kwa wakati na wengine wajitokeze kukopa.




Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Justina Mashiba, akizungumza na waandishi wa habari kwenye ukumbi wa Idara Maelezo jijini Dodoma jana alipoelezea majukumu na mafanikio ya mfuko huo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## UCSAF yaingia mkataba kufikisha huduma vijiji 3,654

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ILI kuimarisha huduma za mawasiliano nchini Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umeingia mikataba ya kufikisha huduma katika kata 1,242 zenye vijiji 3,654 na wakazi 15,130,250.

Mtendaji Mkuu wa Mfuko huo, Justina Mashimba, alibainisha hayo jana jijini hapo alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mfuko huo kwa waandishi wa habari.

Aidha, alisema pia minara 1,087 yenye vijiji 3,378 na wakazi 13,320,750 inatarajiwa kujengwa nchini.

"Utekelezaji unaendelea katika minara 155 yenye vijiji 276 na wakazi 1,809,500, ruzuku iliyotolewa kufanikisha kazi hii ni Sh. bilioni 199,"alisema.

Kadhalika, alisema mradi mwingine ni ule wa kimkakati wa Zanzibar wa minara 42 katika shehia 38 na ruzuku iliyotolewa ni Sh. bilioni 6.9.

Kuhusu mradi wa kupeleka vifaa vya TEHAMA, alisema jumla ya shule 811 nchini zimefikiwa hadi sasa.

"Kwa mwaka wa fedha 2022/23, shule 150 zitafikishiwa vifaa vya TEHAMA, bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/23 ni Sh. bilioni 1.9," alisema.

Aidha, alisema mradi wa kupeleka vifaa maalum vya kujifunzia kwa shule zenye watoto wenye mahitaji maalum shule 16 zimefikishiwa vifaa vya TEHAMA ambavyo ni pamoja na runinga, nukta nundu, mashine za kisasa, kompyuta mpakato, printa ya nukta nundu.

Alisema shule zitakazonufaika ni pamoja na Shule ya Sekondari ya Mpwapwa (Dodoma), Sekondari ya Mkolani (Mwanza), Sekondari ya Kashaulili (Mpanda-Katavi), Sekondari ya Morogoro (Morogoro).

Zingine ni Sekondari ya Shinyanga (Kishapu-Shinyanga), Sekondari ya Wavulana Songea (Songea), Sekondari ya Kazima (Tabora) na Sekondari ya Haile Selassie (Mjini Magharibi) ambapo gharama zikazotumika ni Sh. milioni 575.

Kuhusu kufungwa kwa mtandao wa intaneti maeneo ya wazi alisema maeneo sita yamenufaika na mradi huo.





# Madereva malori wafunga barabara kisa faini za usiku

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHUGHULI za usafiri na usafirishaji katika barabara ya Isyonje-Makete zimekwama kwa zaidi ya saa saba baada ya barabara hiyo kufungwa na madereva wa malori ya kusafirisha viazi mviringo.

Madareva hao walikuwa wakishinikiza maofisa wa halmashauri wanaowatoza faini usiku kuondolewa.

Madereva hao walifunga barabara hiyo juzi wakidai kuwa kuna baadhi ya maofisa wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wamekuwa wakiwasimamisha nyakati za usiku na kuwatoza faini kwa kisingizio kuwa wamekuwa wakizidisha ujazo wa magunia ya viazi maarufu kwa jina la lumbesa.

Wakizungumza na waandishi wa habari, madereva hao walisema wamekuwa wakinyanyaswa na maofisa hao na wakati mwingine wamekuwa wakiwadaiwa rushwa ili wawaachie jambo ambalo limekuwa likiwakera.

Mmoja wa madereva hao, Agrey Ndewesi, alisema maofisa hao wamekuwa wakionekana barabarani nyakati za usiku pekee jambo ambalo limekuwa likiwatia wasiwasi kuwa kuna uwezekano ni wanakuwa hawajatumwa na serikali.

**Wanatusumbua sana hawa maofisa, wanatusimamisha humu barabarani na wanatudai rushwa, kwa hiyo tumeona njia pekee ya kujitetea ni kuifunga barabara hii ili wahusika waje watusikilize.**

Alisema wanaposafirisha viazi hivyo wanakuwa tayari wameshalipa ushuru wa serikali ambao huwa wanalipa Sh. 1,000 kwa gunia moja lakini wanapofika tena kwenye maeneo hayo wanawakuta tena maofisa hao.

"Wanatusumbua sana hawa maofisa, wanatusimamisha humu barabarani na wanatudai rushwa, kwa hiyo tumeona njia pekee ya kujitetea ni kuifunga barabara hii ili wahusika waje watusikilize," alisema Ndewesi.

Naye Abushiri Ilala alisema: "Maofisa hao wamekuwa wakikamata wanaozidisha ujazo, lakini ukiangalia hii mifuko yetu hatujazidisha ujazo popote na ndio maana tumeamua kuomba msaada wa serikali ije itusikilize."

Alisema wao wakiwa mashambani wamekuwa wakijaza viazi kwenye mifuko na kuishona kwa kufuata ujazo halisi lakini wakati wa kusafirisha mifuko huwa inalegea na kuonekana kama lumbesa.

Alisema baada ya kuona wanasumbuliwa na maofisa hao waliwaomba wawapelekee mizani ili wapime kujiridhisha kama kweli wamezidisha ujazo lakini maofisa hao wamekuwa wakiwagomea huku wakiendelea kuwasumbua.

"Tuliwaambia kwamba wakipima wakakuta magunia yetu yamezidi uzito wa kilo 105 watutoze faini na wakikuta ujazo uko sawa watuache tuendelee na biashara zetu," alisema Ilala.

Kitendo cha kufungwa kwa barabara hiyo kilimlazimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Stephen Katemba, kufika katika eneo hilo kwa ajili ya kuwasikiliza madereva hao na kusuluhisha mgogoro huo.

Katemba alisema ujazo ambao aliuona kwenye mifuko hiyo ulikuwa haujazidi na hivyo madereva hao walikuwa hawastahili kutozwa faini ya aina yoyote.

Aliwataka madereva hao kuendelea kuzingatia sheria kwa kutozidisha ujazo ili kuepuka kusumbuana na maofisa wa serikali barabarani kama ambavyo ilitokea.

"Huu ujazo wa sasa haujazidi sana, hapa mfuko ulipofikia ndio eneo ambalo mnatakiwa kuishia kujaza na mkizidi hapa mtakuwa mmevunja sheria, kwa sasa nawaruhusu mwendelee na safari maana hapa mmekwamisha shughuli za watu wengi," alisema Katemba.

Hata hivyo Jeshi la Polisi Wilaya ya Mbeya, lilifika katika eneo hilo kwa ajili ya kulinda usalama ambapo Mwakilishi wa Mkuu wa Polisi Wilaya ya kipolisi Mbalizi, Mkaguzi wa Polisi Richard Maiga aliwataka madereva hao kuacha kujichukulia sheria mkononi.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akisalimiana na wanafunzi wa Shule ya Msingi Ilomba iliyoko Kata ya Isyeisye jijini Mbeya alipokwenda kukabidhi msaada wa madawati 100 jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Dk. Tulia atoa msaada wa madawati 100

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TATIZO la wanafunzi wa Shule ya Msingi Ilomba iliyoko Kata ya Isyesye jijini Mbeya kukosa madawati na wengine kukaa chini, limepungua baada ya kupatiwa msaada wa madawati 111 na wadau mbalimbali.

Madawati hayo yametolewa na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson pamoja na baadhi ya wadau akiwamo Diwani wa Kata ya Isyeseye, Ibrahimu Ipwani.

Dk. Tulia alikabidhi madawati 100 jana na kuahidi kupeleka mengine 60 ili kumaliza tatizo hilo ambalo limekuwa likiisumbua shule hiyo kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi.

Alisema alitoa madawati hayo kutokana na maombi ya uongozi wa shule hiyo ambao ulimwomba asaidie kutatua tatizo hilo la wanafunzi kukaa chini.

"Nimeleta madawati haya 100 kwa sababu ndiyo hesabu ambayo nilikuwa nimepewa, lakini kwa sasa nimeamua kuagiza mengine 60 ambayo bado yanafeli ili yaendelee kutengenezwa," alisema Dk. Tulia.

Hata hivyo Dk. Tulia aliwataka watu wote waliowahi kusoma kwenye shule hiyo kushiriki kuikarabati ili irejee katika hadhi yake ya awali ambayo ilikuwa nayo. Alisema ukarabati huo unatarajiwa kuanza Machi kwa kufukia mashimo yaliyomo kwenye baadhi ya madarasa na kumwaga changarawe nje ili kuondoa matope ambayo yamekuwa yakiwafanya wanafunzi kuwa wachafu.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya, Afley Nsomba, alimshukuru Dk. Tulia pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo mkoani humo kwa kuendelea kushiriki kuboresha miundombinu ya elimu.

Alisema ujenzi wa miundombinu hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho ya mwaka 2020/2025 ambayo inasisitiza miundombinu ya elimu kuboreshwa.

## Askari polisi waliofanya vizuri watunukiwa vyeti, zawadi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya limewatunuku vyeti na zawadi mbalimbali askari wake waliofanya vizuri kwenye utendaji kazi mwaka 2022 kama motisha ya kuwafanya waongeze bidii kwenye utendaji kazi wao.

Zawadi hizo zilikabidhiwa kwa askari hao na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera ambaye ndiye alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla hiyo iliyofanyika kwenye viwanja vya Jeshi la Polisi Kikosi cha Kutuliza Ghasia.

Homera alilipongeza Jeshi la Polisi la mkoa huo kwa kuimarisha ulinzi wa raia na mali zao katika kipindi hiki ambapo alisema matukio ya uhalifu yamepungua kwa kiasi kikubwa katika mkoa huo ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Aliwataka askari hao kuendelea kushirikiana kwenye utendaji kazi wao ili kuhakikisha hali ya utulivu inaendelea kuwapo katika mkoa huo na kuwafanya wananchi kufanya kazi zao kwa amani.

Vilevile aliwataka maofisa wa jeshi hilo wenye vyeo mbalimbali kuendelea kudumisha nidhamu wakati wa kutekeleza majukumu yao ili kuepuka migogoro isiyokuwa na maana ndani ya jeshi hilo.

"Endeleeni kufanya kazi kwa weledi na kutofanya mambo mabaya ambayo yatasababisha kuchafua taswira ya jeshi letu, kwa sasa mnafanya kazi nzuri sana ambayo inatusaidia mkoa wetu kuendelea kuwa na utulivu," alisema Homera.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alisema askari waliochaguliwa kupata zawadi hizo ni wale ambao walishiriki kwenye matukio makubwa ndani ya mkoa huo.

Alisema baadhi yao walishiriki kukabiliana na majambazi na wengine walishiriki kukamata silaha haramu ambazo zilikuwa zinamilikiwa na wahalifu katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.



## Mkutano wa 10 Baraza la Wawakilishi kuanza kesho

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUTANO wa 10 wa Baraza la 10 la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza kesho ambapo masuala mbalimbali yatajadiliwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Katibu wa Baraza hilo, Raya Issa Mselem, alisema miongoni mwa shughuli za mkutano huo ni uwasilishwaji wa ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi 2022/2023.

Alisema pia kutakuwa na uwasilishwaji wa miswaada ya sheria ikiwamo Muswada wa Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar na mambo mingine yanayohusiana na hayo.

Alisema pia kutakuwa na taarifa ya wabunge watano wanaoliwakilisha baraza hilo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, alisema ripoti ya mapendekezo ya mwelekeo wa mpango wa taifa nayo itawasilishwa pamoja na maswali 170 ambayo yataulizwa na kujibiwa.

**Alisema pia kutakuwa na uwasilishwaji wa miswaada ya sheria ikiwamo Muswada wa Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar na mambo mingine yanayohusiana na hayo.**

# Mabadiliko tabianchi yaleta athari kwenye udongo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MTAALAMU wa udongo kutoka Taasisi ya Utafiti ya Kilimo Zanzibar (ZARI), Masoud Salamu Saidi, amesema kuwa athari za mabadiliko ya tabia ya nchi zimesababisha udongo kuathirika kutokana na maji ya bahari kupanda katika maeneo ya kilimo.

Akizungumza jana na Nipashe Visiwani Zanzibar, alisema ili kukabiliana na hali hiyo lazima kuhifadhi rasilimali za misitu na kuacha kukata miti ikiwamo mikoko ambayo inasaidia kuzuwia mmong'onyoko wa ardhi.

Alisema udongo ni kiumbe hai ambacho kinahitaji kulindwa na kuhifadhiwa na moja ya njia ya kulinda ni kuhifadhi mazingira na maliasili kwa sababu misitu ni nyenzo za kuboresha udongo.

Alisema ili kuuhifadhi udongo usiathiriwe, wakulima kulima mazao tofauti na kuacha kuvuna mazao ambayo hayajakomaa, kuepusha matumizi ya kemikali nyingi ikiwamo za kuulia magugu.

"Ardhi ukiitumia vizuri na kulima kilimo stahiki kwa kutotumia mbolea zenye kemikali utakuwa umehifadhi ardhi na wakulima watapata mazao mengi zaidi,"alisema.

Aidha, alisema hakuna utafiti uliofanyika ambao unaonesha kwa kiasi gani udongo wa Zanzibar ulivyoathirika lakini athari zipo kutokana na uvamizi wa ujenzi katika maeneo ya kilimo.

Alisema udongo wa Zanzibar ni mzuri kwa shughuli za kilimo na hakuna zao ambalo haliwezi kuota Zanzibar.

Alisema maeneo mengi ya kilimo Zanzibar yamevamiwa na shughuli za ujenzi hali ambayo imesababisha kuwa na maeneo madogo kwa ajili ya kilimo.

Naye Meneja Ufuatiliaji na Tathmini wa Mradi wa Tuhifadhi Maliasili Tanzania kutoka Shirika la USAID Tuhifadhi Maliasili, John Steven Noronha, alisema uhifadhi wa maliasili ikiwamo misitu na wanyama inasaidia katika kuboresha ubora wa udongo.

"Wapo baadhi ya wajasiriamali wanafanya shughuli zao za kilimo cha mboga katika hifadhi za misitu kwa sababu misitu inasaidia katika kufanya udogo kuwa na rutuba nzuri," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), John Chikomo, alisema mabadiliko ya tabianchi ni janga la ulimwengu mzima hivyo ni vyema waandishi wa habari kupaza sauti zao kutoa elimu kupitia taaluma yao ili kukabiliana na athari za mabadiliko hayo.

Alisema iwapo juhudi za kupunguza athari za mabadiliko hayo hazitachukuliwa sekta ya kilimo itaathirika zaidi na kupelekea ukame na njaa.



Mtaalamu wa udongo kutoka Taasisi ya Utafiti ya Kilimo Zanzibar (ZARI), Masoud Salamu Saidi, akizungumza na Nipashe mjini humo kuhusu ubora wa udongo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wenye ulemavu waliofaulu waomba kukutana na Rais

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANAFUNZI wenye ulemavu waliofaulu mitihani yao ya kidato cha nne wamemwomba Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kukutana nao ili kuwafariji.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wanafunzi hao walisema kuwa kila mwaka Rais wa Zanzibar hukutana na wanafunzi wa kidato cha nne na sita waliopata ufaulu wa daraja la kwanza lakini huwa hakuna wanafunzi wenye ulemavu waliopata ufaulu huo.

Walisema kwa matokeo ya mwaka huu wapo wanafunzi wenye ulemavu waliopata daraja la pili na tatu hivyo ni vyema kujumuika nao ili na wao kufarijika.

Abdul-Azizi Khamis Ali ni mwanafunzi mwenye ulemavu, wa kusikia aliyepata ufaulu wa daraja la pili katika masomo ya sayansi katika Shule ya Sekondari ya Dk. John Joseph Magufuli alisema anatamani kuonanana na Rais ili kumweleza matatizo wanayokabiliana nayo katika elimu.

"Na sisi wanafunzi wenye ulemavu tuliofaulu kwa kuendelea na masomo yetu ya kidato cha tano na sita tunatamani siku moja na sisi tutakutana na Rais wetu," alisema mwanafunzi huyo.

Alisema endapo atapata fursa hiyo ya kuonana na Rais atamweleza matatizo makubwa wanayokumbana nayo wanafunzi viziwi katika kupata elimu ni ukosefu wa wakalimani shuleni.

Mwandawa Khamis, Mwenyekiti wa Shirikisho la Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, alisema kuwa licha ya changamoto zilizoko katika kupata elimu lakini wanafunzi wenye ulemavu wanapambana kutafuta elimu.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Juma Salum Ali, alisema kitendo cha wanafunzi wenye ulemavu kufaulu katika mitihani yao ni cha kupongezwa na kupewa zawadi.

Alisema elimu mjumisho imesaidia watoto wenye ulemavu kutofungiwa ndani na kupelekwa shule kwa ajili ya kupata elimu ambayo ndiyo haki yao ya msingi.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa, alisema wizara hiyo inaendelea kuboresha sekta ya elimu ili watoto wote kupata elimu bora.

Alisema serikali kupitia wizara yake inatarajia kuajiri walimu ikiwamo kwa masomo ya sayansi na wa lugha ya alama ili kuwafundisha wanafunzi shuleni.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka Wizara ya Elimu wanafunzi 14 wa shule za serikali Unguja waliofanya mitihani yao ya taifa ya kidato cha nne wanafunzi mmoja ndiyo aliyepata alama ya ufaulu sifuri.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**MICHAEL WILBROD MAEMBE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA SITA CHENYE NAMBA **S.2213/0059/2016** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA USEVYA SEKONDARI MWAKA 2016. YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/59503/2023**

## TANGAZO KWA UMMA

**Kampuni ya Reco Engineering** Company Ltd iliyopo Chang'ombe Dar Es Salaam inawatangazia wateja binafsi na kampuni zilizoleta kazi zao kwetu na hawajaja kuzichukua kwa muda mrefu hata baada ya kukumbushwa kila mara bila mafanikio yoyote kwamba wanapaswa kuja kuchukua kazi zao ndani ya wiki moja kuanzia tarehe ya tangazo hili vinginevyo kampuni haitahusika na upotevu wa mali au uharibifu wowote utakaojitokeza baada tangazo hili.

Tafadhali zingatia ya kwamba wakati wa kuja kuchukua mali yako utapaswa kuja na fomu ya uthibitisho wa kuleta kazi kwetu sambamba na hilo gharama za utunzaji mali zitahusika.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**

**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa wa Njombe**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 07/2023**

**MATIAS MTAVIKODI MLIGO.................Marehemu**

**IBRAHIM MATHIAS MLIGO...............Msimamizi**

**TAARIFA KWA WADAI**
**(Kanuni ya 9 (1) ya Nyongeza ya V ya Sheria ya Mahakimu wa Mahakama Sura ya 11 Rejeo la 2019)**

TAARIFA inatolewa hapa kwa wote wanaodai kuwa na madai yanayohusiana na mali za marehemu mtajwa hapo juu MATIAS MTAVIKODI MLIGO, aliyefia Makowo-Njombe tarehe 05 Septemba 1991, na Mahakama kunipa barua ya usimamizi wa mirathi hiyo mimi IBRAHIM MATHIAS MLIGO siku ya tarehe 08 Februari 2023, hapa sasa wanatakiwa kunipa madai yao kwangu kupitia namba sanduku langu la barua Makowo Ikuna - Njombe au namba ya simu 0624940641 au kuniletea kwa binafsi, ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya kutangaziwa taarifa hii ambapo muda wake utapoisha nitaendelea kukabidhi mali za marehemu kwa warithi wanaostahili, nikizingatia tu madai ambayo nitakuwa nimearifiwa.

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA, MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 263 YA MWAKA 2022.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU AUGUSTINO LYATONGA MREMA**
**PETER AUGUSTINO MREMA ..................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu,wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 30 mwezi wa Machi, 2023.

Imesainiwa Dar es Salaam, leo tarehe 16 mwezi wa January, 2023

NAIBU MSAJILI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN NOEL HAULE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye jina **JOSEPH GASPER NGONYANI** namba za usajili **T302ANK** aina ya **DONG FANG,** Chassis No.**98DF00060,** Engine No.04011. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/57185/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CRISPO LUDALA CHIFU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 630 AHK MITSUBISHI PICK UP.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Control No: **9910836207992.**

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**

**LAND CASE NO. 4 OF 2022**

**GLADNESS EDWARD SAM (Administrator)**
**Of Edward Heldgard Sam ......................PLANTIFF**

**VERSUS**

**PRIDE TANZANIA-MOSHI BRANCH....................................1st DEFENDANT**
**GRM AUCTIONEER & COURT BROKER..............................2nd DEFENDANT**
**ROBERT KIMARO........................3rd DEFENDANT**

**TO: 1.PRIDE TANZANIA-MOSHI BRANCH**
**2. GRM AUCTIONEER & COURT BROKER**

**NOTICE FOR MENTATION,**

**TAKE NOTICE:** That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 14th February 2023 at 09:00 am before Honourable Judge in charge.
**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this 15th day of December, 2022

DEPUTY REGISTRAR

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0745 700 710.***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika na malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## TANGAZO


WIZARA YA NISHATI
TANESCO
Rural Energy Agency
REA
Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
TUKIO LA UTIAJI SAINI MIKATABA YA
KUIMARISHA GRIDI YA TAIFA NA UMEME VIJIJINI.
14/02/2023
SAA 4 ASUBUHI
TUTAKUWA MUBASHARA
TBC1
UTV
ITV
MAELEZO TV
GRIDI IMARA | UMEME IMARA
#Tupokazini

# KILI MARATHON YATANGAZA RATIBA YA UGAWAJI NAMBA

**Na Mwandishi Wetu**

Waandaaji wa mbio za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon, wametangaza utaratibu wa uchukuaji namba na fulana ('vesti') za kukimbilia kwa waliojisajili.

Hatua hii inakuja baada ya waandaaji hao kutangaza kufungwa kwa usajili wa mbio hizo kwani nafasi zilishajaa kwa mbio za KM 42 na 21 kabla ya Februari 6, mwaka huu ambayo ilikuwa tarehe ya mwisho ya kujisajili.

Taarifa iliyotolewa na waandaaji hao ilieleza kuwa zoezi hilo litaanzia jijini Dar es Salaam Jumamosi na Jumapili wiki hii katika viwanja vya Mlimani City kuanzia saa sita mchana hadi saa 12 jioni.

Baada ya Dar es Salaam, zoezi hilo litahamia Arusha katika hoteli ya Kibo Palace Februari 21 na 22, mwaka huu kuanzia saa nane mchana hadi saa 11 jioni.

Kituo cha mwisho ni Moshi Mjini ambapo zoezi hilo litafanyika Februari 23 saa sita mchana hadi saa 12 jioni), Februari 24 kuanzia saa 4 asubuhi hadi saa 12 jioni na Februari 25 kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa kumi na moja jioni) katika Uwanja wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU).

Waandaaji hao wametoa wito kwa washiriki kuzingatia muda katika kila kituo ili kuepusha usumbufu na pia walitoa wito kwa wanaowachukulia washiriki wengine namba zao wahakikishe wanaenda na nakala ya kitambulisho au barua kutoka kwa mshiriki halisi.

"Ni matumaini yetu kuwa washiriki watajitokeza kwa wingi jijini Dar es Salaam na Arusha ili kupunguza msongamano Mjini Moshi," ilisema sehemu ya taarifa ya waandaaji hao.

Waandaaji hao pia wamesisitiza kuhusu hatua zitakazochukuliwa dhidi ya watu wanaodaiwa kuuza tiketi mtandaoni kwa njia isiyo halali. "Watu hawa watachukuliwa hatua za kisheria kwa sababu ni marufuku kuuza tiketi bila idhini ya waandaaji na hata hivyo usajili umeshafungwa," ilisema taarifa hiyo na kuongeza:.

"Watakaokimbia na namba feki zikiwamo za miaka iliyopita pia watachukuliwa hatua ikiwamo kuondolewa mashindanoni, kufutiwa matokeo na pia kufungiwa kushiriki Kilimanjaro Marathon kabisa."

Wadhamini wa mbio hizi ni pamoja na Kilimanjaro Premium Lager - Km. 42 (Mdhamini Mkuu), Tigo - Km. 21 (Half Marathon), Grand Malt - Kilometa tano Fun Run, wadhamini wa meza za maji - TPC Sugar, Simba Cement, Kilimanjaro Water, Total Energies na wasambazaji maalumu Kibo Palace Hotel, CMC Automobiles, KK Security na Keys Hotel.

## INAKUWA HIVI...



Kocha Maalim Seif, akitoa mifano kwa makipa wa timu ya Masala wakati wa mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KMKM bado yatesa kileleni Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya KMKM imeendelea kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar kwa kuwa na alama 44 ikifuatiwa na mpinzani wake wa karibu, KVZ FC yenye pointi 40 huku nafasi ya tatu ikishikiliwa na Mlandege FC yenye alama 38.

Ligi hiyo ambayo itaendelea Alhamisi wiki hii huku timu zote zikiwa tayari zimecheza michezo 20, kila moja imebakisha michezo 10 kabla ya msimu kumalizika.

Kwa mujibu wa baadhi ya makocha wa Klabu za Ligi Kuu Zanzibar, wamesema ligi hiyo msimu huu, imezidi kuwa ngumu ikilinganishwa na msimu uliopita.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu ya KMKM, Ame Msimu, yeye alisema kwa upande wa tathmini yake katika michezo 20 iliyochezwa timu zote zimeonyesha upinzani mkali hata zilizofungwa.

Alisema msimu huu hakuna timu iliyoruhusu kufungwa mabao mengi zaidi hata zile ambazo zinaburuza mkia.

"Tupo katika mbio za ubingwa, lakini ligi bado ngumu mno, michezo 10 iliyobaki kwa kila timu, lolote linaweza kutokea kwa aliyejuu na aliye chini kabisa ya msimamo," alisema.

Kwa upande wa Kocha wa timu ya Zimamoto, Moh'med Hilali 'Teddy', alisema ugumu wa msimu huu umetokana na klabu zote kufanya maandalizi ya mapema hasa katika kusajili wachezaji wazuri.

Alisema mara nyingi walizoe kuona viwango vya wachezaji wa Zanzibar vikilingana ambapo kwa msimu huu imekuwa tofauti na kuleta ushindani wa hali ya juu.

"Msimu huu ni mgumu, yale mazoea ambayo tulikuwa tunayaona kwa wachezaji hakuna tena, kila timu na mchezaji ana mbinu zake na kila mwalimu anakuwa na mfumo tofauti kulingana na ugumu wa mechi, hivyo mpaka sasa tumebakisha michezo 10 hakuna timu ambayo inatabiriwa kuwa bingwa licha ya KMKM kupigiwa upatu mkubwa na wadau wa soka,"alisema.

Timu ambazo zipo katika hatari ya kushuka daraja ni Taifa Jang'ombe ambayo inaburuza mkia ikiwa na alama 10, ikifuatiwa na Dulla Boys ambayo ipo nafasi ya 15 na pointi zake 12, nafasi ya 14 ni timu ya Black Sailor yenye alama 14 na timu ya 13 ni Polisi ikiwa na alama 16.

## Serikali yabariki Super Women Boxing Night

**Na Saada Akida**

KAIMU Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo nchini, Ally Mayay, amebariki zoezi la upimaji afya kwa wanamichezo wote kuelekea katika pambano la wanawake Super Women Boxing Night linalotarajiwa kupigwa Machi 11, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

Mayai amewapongeza waandaaji, Kwame Sports, ikiwa ni mara ya kwanza kufanyika nchini pambano kubwa la ngumi za kulipwa ambalo litawakutanisha wanawake watupu huku likiambatana na zoezi la upimaji afya kwa wanamichezo wote litakalosimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Mayay alisema amewapongeza waandaaji hao kutokana na tukio hilo ikiwamo zoezi la kupima afya linalotarajiwa kufanyika Machi 8, mwaka huu, katika Ukumbi wa Diamond Jubilee huku akiwataka wadau kuendelea kijitokeza kusapoti pambano hilo.

"Niwapongeze sana shirikisho kwa tukio hilo ambalo linathibitisha tasnia ya michezo yenyewe kwa sababu sasa hivi ngumi ni biashara, Watanzania wengi uchumi unaowazunguka ni kupitia mchezo huu wa ngumi.

## New Generation yanyolewa Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKONGWE wa Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar, timu ya New Generation, imeambulia kichapo cha mabao 4-2 dhidi ya Pds Princess katika mchezo wa kwanza wa raundi ya pili wa ligi hiyo uliochezwa juzi katika Dimba la Mau B.

Licha ya kichapo hicho, New Generation imeendelea kuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 18 huku Pds ikiwa na pointi 12 katika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar inayoshirikisha jumla ya timu saba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa New Generation, Ahmad Ali Bakari, alisema kupoteza kwao mchezo huo, kumetokana na kuzidiwa mbinu na wapinzani wao.

Alisema wapinzani wao walicheza vizuri katika kipindi cha kwanza ambacho walivuna magoli matatu hivyo ilikuwa kazi ngumu kwao kipindi cha pili kutokana na kucheza kwa kujilinda zaidi kuliko kushambulia, hivyo kwa sasa wanajipanga kwa ajili ya mchezo ujao dhidi ya Dunga Queens.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**OSIMHEN AWANIWA LIVER**
LIVERPOOL wameingia kwenye kinyang'anyiro cha kuwania saini ya Victor Osimhen kutoka Napoli. Mshambuliaji huyo wa Nigeria mwenye umri wa miaka 24, pia anasakwa na Manchester United. ***(Fichajes)***

**RAYA AWINDWA CHELSEA**
CHELSEA ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia mlinda mlango wa Brentford na Hispania, David Raya, mwenye umri wa miaka 27. ***(Football.London)***

**EZZALZOULI NAYE ANYATIWA**
CHELSEA pia inataka kumsajili winga wa Barcelona na Morocco, Abde Ezzalzouli. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kwa sasa yuko kwa mkopo Osasuna. ***(Mundo Deportivo)***

**VERBRUGGEN ATAKIWA LIVER**
LIVERPOOL inataka kumsajili mlinda mlango wa Anderlecht, Bart Verbruggen mwenye umri wa miaka 20. ***(Sun)***

**PICKFORD MKATABA MPYA**
KOCHA mpya wa Everton, Sean Dyche, amempa umuhimu mkubwa mlinda mlango wa England, Jordan Pickford, mwenye umri wa miaka 28 na anamtaka kusaini mkataba mpya katika klabu hiyo**. *(Sun)***

**MARSCH NA SOUTHAMPTON**
KOCHA wa zamani wa Leeds United Jesse Marsch, huenda akaajiriwa Southampton baada ya kuondoka kwa Nathan Jones, wiki moja baada ya kuondoka Elland Road. ***(Athletic)***

**FURUHASHI LULU PALACE**
KLABU ya Crystal Palace inamfuatilia mshambuliaji wa Celtic na Japan, Kyogo Furuhashi, mwenye umri wa miaka 28. ***(Football Insider)***

**KAMADA SASA AGOMBEWA**
KALBU ya Newcastle United ipo mbele ya Liverpool na Barcelona katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa kati wa Eintracht Frankfurt na Japan, Daichi Kamada mwenye umri wa miaka 26. ***(CaughtOffside)***

**GALLARDO KWA LEEDS**
KLABU za Southampton na Leeds United zinamtaka kocha wa Argentina, Marcelo Gallardo mwenye umri wa miaka 47 kuwa kocha wao mpya. ***(Football Insider)***

**PEDRO ATAJWA WEST HAM**
MSHAMBULIAJI wa Flamengo na Brazil, Pedro mwenye umri wa miaka 25, yuko kwenye rada za West Ham. ***(Fichajes)***



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND SASA HATIHATI KUIVAA ARSENAL J'MOSI

**Guardiola asema hajui ni muda gani atakaa nje, ikiwa hayuko tayari tutacheza...**

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola hana uhakika kuhusu ukubwa wa jeraha la Erling Haaland kabla ya mechi muhimu ya Manchester City dhidi ya Arsenal.

City walirejea katika njia ya mbio za ubingwa kwa kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Aston Villa kwenye Uwanja wa Etihad Jumapili.

Huku Arsenal wakiwa wamepoteza pointi dhidi ya Brentford Jumamosi, ushindi kwenye Uwanja wa Emirates siku ya Jumatano utaifanya City kukwea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu lakini kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa, ingawa 'Washikabunduki' bado watakuwa na mchezo mkononi.

Bado haijulikani kama Haaland atakuwa fiti kwenye mchezo huo baada ya mshambuliaji huyo, ambaye alimsaidia Ilkay Gundogan kufunga bao la pili la City, kutolewa nje wakati wa mapumzikoni.

"Sijui, ni muda gani atakaa nje," alisema Guardiola, ambaye alikuwa akisimamia mechi yake ya 250 ya Ligi Kuu ya England akiiambia Sky Sports alipoulizwa kuhusu Haaland.

"Ikiwa hayuko tayari, tutacheza nyingine. Tunatumaini yuko tayari, kama kila mtu. Tutaona ni nini."

"Uwapo wake ni mzuri sana," aliongeza Guardiola. "Tunapokuwa hatuna shinikizo kwenye mpira, mpinzani anapokuwa na safu ya juu, tutaweza kumpata zaidi. Tutafanya hivyo siku zijazo."

"Tutaona Ligi Kuu itakapokamilika. Tutaenda London kujaribu kushinda mchezo.

"Timu moja inapofikisha pointi 50 ni kwa sababu wanafanya vizuri sana, hatimaye walipodondosha pointi sisi tulikuwapo kupunguza tofauti."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 472,

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT
YA MECHI - 13
TZS.
248,672,790
IMEPATA MSHINDI

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI: BARCA ITAIMARIKA ZAIDI



**BARCELONA, Hispania**

XAVI amesisitiza kwamba bado kuna mengi zaidi yanakuja kwa Barcelona baada ya timu yake kushinda bao 1-0 dhidi ya Villarreal na kuongoza msimamo kwa tofauti ya pointi 11 kwenye kilele cha LaLiga.

Barcelona waliendelea na rekodi yao nzuri ya mwaka huu kwa ushindi wa 11 mfululizo kutokana na bao la Pedri la kipindi cha kwanza.

Miamba hao wa Katalunya walijitahidi kuwa kwenye kiwango bora, huku Robert Lewandowski akipiga mashuti mara tatu ambayo yaliokolewa na Pepe Reina.

Samuel Chukwueze alimfunga Marc-Andre ter Stegen, lakini bao hilo lilikataliwa haraka kwa sababu ya kuotea.

"Kuna pointi nyingi zilizosalia kuchezea," aliiambia Movistar+.

"Mbio za kiwango tunazocheza ni za kushangaza, lakini bado tunaweza kuboresha baadhi ya mambo.

"Villarreal walitaka kumiliki mpira leo (juzi), na walitubana. Tulikosa pasi nyingi za mwisho."

Barcelona wameandikisha ushindi mara saba katika michezo 21 ya LaLiga msimu huu, sawa na jumla yao ya juu zaidi katika msimu mzima katika historia ya mashindano hayo.

Wameruhusu mabao saba pekee ya LaLiga katika kampeni zote, ambazo ni sita pungufu kuliko timu yoyote katika ligi tano bora za Ulaya.

Bao la Pedri dakika ya 18 lilikuwa la sita msimu huu kwenye ligi, mabao manne kati ya hayo alifunga Barca katika ushindi wa 1-0.

# Giroud kuendelea kuichezea Ufaransa

**MILAN, Italia**

MFUNGAJI bora wa mabao wa Ufaransa, Olivier Giroud, ameamua kutostaafu soka la kimataifa na anatumaini bado ataendelea kukichezea kikosi hicho cha kocha, Didier Deschamps.

Mshambuliaji huyo wa AC Milan mwenye umri wa miaka 36, aliaminika kuwa angeacha kuichezea 'Les Bleus' hao baada ya kufungwa kwa mikwaju ya penalti na Argentina katika fainali ya Kombe la Dunia Desemba 18, mwaka jana.

Hata hivyo, Giroud anahisi bado ana mengi ya kuiwezesha nchi yake kushiriki kikamilifu, na mtu ambaye amefunga mabao 53 katika michezo 120 atalenga kuwa sehemu ya kundi linaloelekea katika kampeni zijazo za ubingwa wa Ulaya.

Huenda ikasaidia sababu ya Giroud kwamba Karim Benzema wa Real Madrid amestaafu kuichezea Ufaransa, baada ya kukosa fainali za Qatar 2022 kutokana na jeraha.



Akizungumza na mtangazaji wa Kituo cha Televisheni cha France 2, Giroud alisema: "Hapana, hapana, bado naweza kuendelea kuichezea Ufaransa.

"Siko tayari kutundika daluga, kuvua jezi hii ya bluu ambayo iko karibu na moyo wangu.

"Nina motisha ya kuendelea na hali ya mwili pia, najisikia vizuri. Kwa sasa bado naweza kuchaguliwa kuichezea timu ya Ufaransa. "

Kocha Mkuu, Deschamps, ambaye alibakizwa baada ya kuamua yeye pia hakuwa tayari kuondoka Les Bleus, aliona Giroud akifunga mabao manne wakati wa mbio za Kombe la Dunia za Ufaransa.

Walifika pungufu tu ya kutetea ubingwa kwa mafanikio, huku Giroud akinyakua ushindi muhimu wa robo fainali dhidi ya England miongoni mwa mchango wake.

Giroud alimpita Thierry Henry na kuwa mfungaji bora wa Ufaransa wakati wa kampeni za Kombe la Dunia, akimzidi mshambuliaji huyo wa zamani wa Arsenal na Barcelona aliyefunga mabao 51 katika timu ya taifa.

Nahodha Hugo Lloris, pamoja na kipa mwenzake Steve Mandanda na beki Raphael Varane, walistaafu kutoka Ufaransa baada ya Kombe la Dunia.

Ufaransa wanaanza kampeni yao ya kufuzu Euro 2024 kwa mechi za Kundi B dhidi ya Uholanzi na Jamhuri ya Ireland Machi.

# SIMBA YAGEUKIA MASTRAIKA MECHI RAJA CASABLACA CAF

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupoteza mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ugenini dhidi ya Horoya AC ya Guinea, Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda ameweka wazi kazi kubwa wanayoifanya kwa sasa ni kuwapa programu maalum washambuliaji wao kuelekea mechi zijazo za michuano hiyo.

Safu ya ushambuliaji ya Simba inaongozwa na Jean Baleke, Moses Phiri na John Bocco ambaye alikosa nafasi nyingi za wazi katika mchezo uliopita.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa simu, Mgunda alisema wameona madhaifu ya kikosi chao hasa safu yao ya ushambuliaji kwa kutokuwa makini na kukosa utulivu hivyo kuandaa programu maalum katika mazoezi.

Alisema katika programu hiyo ni pamoja na kuwajenga kisaikolojia wachezaji wao na anaimani kubwa ya kufanya vizuri katika michezo iliyosalia ukiwamo watakaocheza nyumbani dhidi ya Raja Casablanca Jumamosi.

"Ni mechi ngumu na ushindani mkubwa, ukizingatia tumetoka kupoteza, lakini tutakuwa nyumbani na tunahitaji kupata matokeo mazuri katika mchezo huo dhidi ya Raja Casablanca.

"Kwa washambuliaji wetu inawalazimu kuwa na umakini na utulivu kichwani ili kufikia malengo ya kukusanya pointi tatu kila mechi tutakayocheza nyumbani," alisema Mgunda.

Alisema wamewasoma wapinzani wao katika mchezo uliopita walipocheza na Vipers ya Uganda katika mechi ya kwanza, kwa kuona ubora na madhaifu ya Raja Casablanca.

"Ni timu nzuri, lakini tunatarajia kupata matokeo mazuri katika ardhi ya nyumbani, ninaimani wachezaji wetu wako vizuri na tunaendelea na maandalizi katika mchezo wetu huo," alisema Mgunda.

Simba wanarejea nchini leo na kuingia kambini moja kambini kujiandaa na mchezo wa pili wa hatua ya makundi ya ligi hiyo dhidi ya Raja Casablanca utakaocheza Februari 18, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

SOKA...



Vijana wanaolelewa katika Kituo cha Michezo cha JK Park jijini Dar es Salaam wakiwania mpira wakati wa mazoezi katika viwanja hivyo jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KOCHA US MONASTIR AIVULIA KOFIA YANGA

INATOKA UK. 24

dakika ya 32.

Baada ya mechi hizo za kwanza, TP Mazembe imekaa kileleni ikiwa na pointi tatu mabao matatu, Monastir ikishika nafasi ya pili kwa pointi tatu na mabao mawili, Yanga ikiwa nafasi ya tatu bila pointi lakini mabao mawili ya kufungwa huku Real Bamako ikishika mkia ikiwa haina pointi, bao moja la kufunga na kuruhusu matatu.

## SERIKALI YAGEUKIA SAKATA MKATABA

INATOKA UK. 24

fedha zake za usajili ili kuvunja mkataba, jambo ambalo waajiri wake walidai kuzirejesha kwa ni kinyume na utaratibu kimkataba.


,189,430

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/02/23 | 20:00 | Omonia Nicosia vs Apoel Nicosia | 2.55 | 3.16 | 2.55 |
| 02. 15/02/23 | 22:30 | Arsenal vs Manchester City | 2.71 | 3.24 | 2.48 |
| 03. 15/02/23 | 22:45 | Motherwell vs St Mirren | 2.36 | 3.23 | 2.93 |
| 04. 15/02/23 | 22:45 | Preston vs Luton Town | 2.53 | 3.13 | 2.73 |
| 05. 15/02/23 | 23:00 | Borussia Dortmund vs Chelsea | 2.37 | 3.37 | 2.77 |
| 06. 16/02/23 | 06:05 | Club Necaxa vs UNAM Pumas | 2.45 | 3.35 | 2.71 |
| 07. 16/02/23 | 20:45 | RB Salzburg vs Roma | 2.73 | 3.23 | 2.53 |
| 08. 16/02/23 | 20:45 | Sporting Braga vs Fiorentina | 2.43 | 3.39 | 2.74 |
| 09. 16/02/23 | 23:00 | Sevilla FC vs PSV Eindhoven | 2.24 | 3.39 | 3.05 |
| 10. 16/02/23 | 23:00 | Sheriff Tiraspol vs Partizan | 2.50 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 17/02/23 | 00:00 | Mirassol SP vs Ituano SP | 2.68 | 2.89 | 2.63 |
| 12. 17/02/23 | 03:30 | Corinthians vs Palmeiras | 3.00 | 2.75 | 2.24 |
| 13. 17/02/23 | 11:45 | Western United vs Wellington Phoenix | 2.70 | 3.23 | 2.53 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 14/02/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:45 | 2567 | AL Riyadh vs Hajer Club | 2.00 | 2.91 | 3.89 |
| 15:50 | 4739 | Al Faisaly (KSA) vs AL Akhdood | 1.62 | 3.40 | 5.35 |
| 15:55 | 4660 | AL Arabi (SA) vs AL Khlood | 2.11 | 2.89 | 3.57 |
| 16:30 | 1843 | RNK Split vs Dinamo Zagreb | 16.62 | 10.39 | 1.06 |
| 16:30 | 3019 | Shabab AL Ahli Dubai Club vs Al Dhafra | 1.18 | 5.80 | 12.43 |
| 16:45 | 4724 | Al Fehaheel vs Al Kuwait SC | 5.61 | 3.95 | 1.50 |
| 17:00 | 3904 | Hyderabad FC vs ATK Mohun Bagan | 2.20 | 3.20 | 3.00 |
| 17:00 | 5657 | Cesena Youth vs Napoli Youth | 2.21 | 3.20 | 2.70 |
| 18:30 | 4782 | Riffa Club vs Al Ahli Manama | 1.96 | 3.22 | 3.58 |
| 19:00 | 5116 | AEL Limassol vs Nea Salamis | 1.84 | 3.38 | 3.84 |
| 22:45 | 1008 | Salford City vs Harrogate | 1.87 | 3.41 | 3.96 |
| 22:45 | 1025 | Newport vs Stevenage | 2.92 | 3.17 | 2.37 |
| 22:45 | 1069 | Notts County vs Barnet | 1.33 | 5.06 | 7.39 |
| 22:45 | 1167 | Colchester vs Walsall | 2.68 | 3.07 | 2.63 |
| 22:45 | 1353 | Port Vale vs Barnsley | 3.02 | 3.32 | 2.24 |
| 22:45 | 1359 | Oxford Utd vs Plymouth | 2.66 | 3.26 | 2.52 |
| 22:45 | 1408 | Norwich City vs Hull City | 1.76 | 3.62 | 4.27 |
| 22:45 | 1699 | Carrick Rangers vs Ballymena Utd | 2.19 | 3.42 | 2.85 |
| 22:45 | 1799 | Dungannon Swifts vs Larne | 8.29 | 4.97 | 1.28 |
| 22:45 | 1951 | Coventry vs Millwall | 2.46 | 3.13 | 2.83 |
| 22:45 | 2092 | Birmingham vs Cardiff | 2.23 | 3.16 | 3.16 |
| 22:45 | 2118 | Carlisle vs Mansfield | 2.33 | 3.17 | 2.98 |
| 22:45 | 2145 | Accrington vs Wycombe | 3.27 | 3.32 | 2.11 |
| 22:45 | 2257 | Cliftonville Belfast vs Portadown FC | 1.16 | 6.41 | 12.41 |
| 22:45 | 2395 | Portsmouth vs Burton | 1.72 | 3.72 | 4.37 |
| 22:45 | 2813 | Forest Green vs Charlton | 2.92 | 3.22 | 2.34 |
| 22:45 | 3169 | Bradford City vs Tranmere | 2.32 | 3.13 | 3.03 |
| 22:45 | 3276 | Stockport vs Crawley Town | 1.38 | 4.57 | 7.35 |
| 22:45 | 3319 | Coleraine FC vs Newry City AFC | 1.33 | 4.79 | 7.08 |
| 22:45 | 3716 | Exeter vs Shrewsbury | 2.15 | 3.27 | 3.22 |
| 22:45 | 3842 | Derby vs Lincoln | 1.45 | 4.26 | 6.53 |
| 22:45 | 3957 | Sutton United vs Swindon Town | 2.26 | 3.17 | 3.12 |
| 22:45 | 4000 | Doncaster vs Barrow | 2.26 | 3.17 | 3.12 |
| 22:45 | 4332 | Wrexham vs Woking | 1.48 | 4.15 | 5.89 |
| 22:45 | 4349 | Leyton Orient vs Rochdale | 1.60 | 3.62 | 5.55 |
| 22:45 | 4360 | Cambridge Utd vs Cheltenham | 2.29 | 3.27 | 2.97 |
| 22:45 | 4505 | Northampton vs AFC Wimbledon | 2.00 | 3.26 | 3.65 |
| 22:45 | 4695 | Bolton vs MK Dons | 1.68 | 3.71 | 4.65 |
| 22:45 | 4711 | Bristol Rovers vs Ipswich | 4.97 | 3.83 | 1.62 |
| 22:45 | 4770 | Sheffield Wed vs Morecambe | 1.25 | 5.56 | 9.93 |
| 22:45 | 5279 | QPR vs Sunderland | 2.32 | 3.27 | 2.92 |
| 22:45 | 5650 | Crewe vs Hartlepool | 2.29 | 3.19 | 3.04 |
| 22:45 | 5701 | Glentoran Belfast vs Linfield Belfast | 2.59 | 3.42 | 2.37 |
| 22:45 | 5731 | Glenavon vs Crusaders Belfast | 4.34 | 4.14 | 1.59 |
| 22:45 | 5736 | Gillingham vs Grimsby | 2.43 | 3.07 | 2.92 |
| 22:45 | 5946 | Fleetwood Town vs Peterborough | 3.28 | 3.33 | 2.11 |
| 23:00 | 4036 | AC Milan vs Tottenham | 2.46 | 3.27 | 2.72 |
| 23:00 | 4085 | Paris St Germain vs Bayern Munchen | 2.53 | 3.67 | 2.42 |
| 23:00 | 5179 | Reading vs Rotherham | 1.98 | 3.28 | 3.72 |
| 23:00 | 5906 | Burnley vs Watford | 1.66 | 3.77 | 4.76 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumanne Februari 14, 2023

Nipashe



UKURASA 21

## Haaland sasa hatihati kuivaa Arsenal J'mosi

# KOCHA US MONASTIR AIVULIA KOFIA YANGA

## ●●●Aitabiria kutisha katika kundi lao, lakini aishangaa kuruhusu mabao ya mipira iliyokufa, Nabi naye asema..

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Yanga, Kocha Mkuu wa US Monastir, Nivic Darko, ameonyesha kuvutiwa na kiwango walichoonyesha wapinzani wao, akisema ni timu nzuri na huenda ikawa ni ngumu zaidi kwenye kundi lao, lakini akionyesha kushangazwa kufungwa kirahisi mabao ya 'mipira iliyokufa'.

Akizungumza nchini Tunisia baada ya kumalizika kwa mechi hiyo iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Olympique Hamadi Agrebi Rades, kocha huyo pia amewasifu wachezaji wake kwa kupata ushindi kwenye mechi ya kwanza ya makundi Kombe la Shirikisho Afrika katika historia ya klabu hiyo.

"Yanga ni timu nzuri, inaweza kuwa ni timu ngumu zaidi kwenye kundi hili, wana wachezaji wenye uzoefu, nawapongeza, lakini wamenishangazwa kufungwa mabao mawili ya mipira ya kutengwa. Lakini nawapongeza vijana wangu kwa sababu ilikuwa ni mechi yetu ya kwanza kucheza kwenye makundi tangu timu hii ianzishwe, tunakwenda hatua kwa hatua mpaka tuone mwisho wake," alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema wamepoteza mechi hiyo, hivyo wanaachana nayo, badala yake wanaangalia mechi ijayo Jumapili dhidi ya TP Mazembe inatakayochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yalikuwa ni mabao ya Mohamed Saghafaoui dakika ya 10 na Boubacar Traore dakika ya 16.

Juzi pia kwenye mechi ya Kundi D, TP Mazembe ilianza vema michuano hiyo baada ya kuichapa Real Bamako ya Mali mabao 3-1 kwenye Uwanja wa TP Mazembe, Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Mabao ya washindi yalifungwa na Jephte Kitambala dakika ya 24, Alex Ngonga dakika ya 38 na Patient Mwamba dakika za majeruhi, huku bao la kufutia machozi la wageni likifungwa na Souleymane Coulibaly

INAENDELEA UK. 23

**WANGU HUU...**



Mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, akimiliki mpira dhidi ya Kiungo wa US Monastir, Mondher Guesmi, katika mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Olympique Hamadi Agrebi Rades jijini Tunis, Tunisia juzi na kumalizika kwa wenyeji kushinda mabao 2-0. **PICHA: YANGA**

## Serikali yageukia sakata mkataba Fei Toto, Yanga

**Na SaadaAkida**

KUTOKANA na mvutano mkubwa uliopo kati ya uongozi wa klabu ya Yanga na kiungo wa timu hiyo, Feisal Salimu 'Feitoto', ambao bado haujapatiwa suluhisho, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo nchini, Ally Mayay, ameibuka na kuwataka kutumia busara kuweza kulimaliza suala hilo.

Mayay ametoa kauli hiyo kutokana na sakata la muda sasa kati ya mchezaji huyo na mabosi wake hali iliyosababisha kuwa nje ya timu hiyo huku akiwa ametangaza kuvunja mkataba na klabu hiyo kabla ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kuweka wazi kwamba bado ni mchezaji halali wa mabingwa watetezi hao wa Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mayay alisema sakata hilo linahitajika busara kubwa kutoka pande zote mbili ili kuweza kulimaliza kutokana na kila upande athirika.

"Nadhani jambo kubwa ni wao kuweza kutumia busara upande wa Yanga na wa Fei ili kuweza kumaliza hili jambo na kufanya mambo mengi yaweze kuendelea kwa sababu kinachotokea kwa sasa ni athari ambazo kila upande umekuwa ukizipata.

"Kila mmoja bado anahitaji kitu kutoka kwa mwenzake kwa sababu Yanga wao watakuwa waathirika kibiashara na wana mkosa mchezaji huyo," alisema Mayay.

Alisema pia mchezaji atakuwa anapata wakati mgumu kutokana na kukosa stahiki zake, lakini hata kipaji chake kwa kuwa muda mwingi amekuwa nje ya timu, hivyo bado wanayo nafasi wote kuweza kutumia busara kumaliza jambo hilo.

Hivi karibuni kiungo huyo alipeleka barua TFF kuomba kurejewa kesi yake katika Kamati ya Hadhi na Haki za Wachezaji ya shirikisho hilo.

Fei Toto ana mgogoro wa kimkataba na waajiri wake tangu mwishoni mwa mwaka jana baada ya kutumia kipengele kinachomtaka kurejesha

INAENDELEA UK. 23



9 770856 541002 >